

**HOTUBA YA WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA
NA MAENDELEO YA MAKAZI, MHESHIMIWA
WILLIAM V. LUKUVI (MB.), AKIWASILISHA
BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA
MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA
2017/18**

Dodoma

Mei, 2017

YALIYOMO

DIRA YA WIZARA	v
DHIMA	v
MADHUMUNI	v
MAJUKUMU	vi
A: UTANGULIZI	1
B: MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2016/17 NA MALENGO YA MWAKA WA FEDHA 2017/18	7
HUDUMA ZA MAENDELEO YA ARDHI	13
HUDUMA ZA UPIMAJI NA RAMANI	33
HUDUMA ZA UPANGAJI MIJI NA VIJJI	39
MAENDELEO YA SEKTA YA NYUMBA	51
HUDUMA ZA KISHERIA NA SERA	60
HUDUMA ZA UTAWALA NA RASILIMALI WATU	63
C: CHANGAMOTO NA MIKAKATI YA KUKABILIANA NAZO	66
D: SHUKRANI	68
E: HITIMISHO	69
F: MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2017/18	70
Fungu 48: Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi	71
Fungu 03: Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi	72

DIRA YA WIZARA

Kuwa na uhakika wa milki za ardhi, nyumba bora na makazi endelevu kwa ajili ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

DHIMA

Kuweka mazingira wezeshi ya kuleta ufanisi katika utoaji wa huduma za ardhi, nyumba na makazi.

MADHUMUNI

- i) Kuimarisha usalama wa milki za ardhi;
- ii) Kuboresha mfumo wa taarifa za kielektroniki za ardhi nchini;
- iii) Kuendeleza utafiti wa vifaa vya ujenzi wa nyumba bora na zenye gharama nafuu kwa ajili ya uendelezaji makazi nchini;
- iv) Kuboresha ushirikiano, mawasiliano na uratibu wa masuala ya kitaifa, kikanda na kimataifa katika sekta ya ardhi;
- v) Kuboresha utendaji na utoaji huduma katika sekta ya ardhi;
- vi) Kutoa huduma na kupunguza maambukizi ya UKIMWI; na

- vii) Kuimarisha utawala bora na kupambana na rushwa.

MAJUKUMU

- i) Kuratibu utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995;
- ii) Kuratibu utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000;
- iii) Kusimamia utawala wa ardhi nchini;
- iv) Kusimamia upangaji, upimaji na uendelezaji miji na vijiji;
- v) Kusimamia upimaji wa ardhi na kutayarisha ramani;
- vi) Kumilikisha ardhi na kuwezesha utoaji wa hatimiliki za kimila;
- vii) Kusajili hatimiliki za ardhi na nyaraka za kisheria;
- viii) Kusimamia uthamini wa mali;
- ix) Kuhamasisha na kuwezesha ujenzi wa nyumba bora;
- x) Kusimamia uendelezaji milki;
- xi) Kusimamia Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya katika utatuzi wa migogoro ya ardhi;

- xii) Kusimamia utunzaji wa kumbukumbu za ardhi;
- xiii) Kusimamia ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali yatokanayo na huduma za sekta ya ardhi;
- xiv) Kuwezesha uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi na kufuatilia utekelezaji wake;
- xv) Kusimamia maslahi na utendaji kazi wa watumishi; na
- xvi) Kusimamia Vyuo, Taasisi na Wakala zilizo chini ya Wizara ambazo ni Vyuo vya Ardhi Tabora na Morogoro, Shirika la Nyumba la Taifa, Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi, Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba na Vifaa vya Ujenzi, Wakala wa Uendelezaji wa Mji Mpya wa Kigamboni, Bodi ya Wataalam wa Mipangomiji, Halmashauri ya Wapima Ardhi, Bodi ya Usajili wa Wathamini na Mfuko wa Fidia ya Ardhi.

**HOTUBA YA WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA
NA MAENDELEO YA MAKAZI, MHESHIMIWA
WILLIAM V. LUKUVI (MB.), AKIWASILISHA
BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA
MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA
2017/18**

A: UTANGULIZI

- 1) *Mheshimiwa Spika*, kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka wa fedha 2016/17 pamoja na ile ya Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu lijadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Fungu Na. **48** na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi, Fungu Na. **3** kwa mwaka wa fedha 2017/18. Vilevile, pamoja na hotuba hii nimewasilisha taarifa ya utekelezaji wa programu na miradi ikijumuisha miradi inayosimamiwa na taasisi, wakala zilizo

chini ya Wizara pamoja na taarifa ya urasimishaji wa makazi nchini.

2) **Mheshimiwa Spika**, awali ya yote naomba kutoa salamu za pole kwako na Bunge lako Tukufu kufuatia kifo cha aliyekuwa Spika wa Bunge la Tisa hayati Samuel John Sitta. Aidha, katika kipindi hiki tumewapoteza wabunge wenzetu wawili ambao ni Mhe. Hafidh Ally Tahir aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Dimani (CCM) pamoja na Mhe. Dkt. Elly Marko Macha aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA). Naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa salamu za rambirambi kwa familia za marehemu, ndugu na wote walioguswa na misiba hiyo. Vilevile, nitumie fursa hii kuwapa pole Watanzania ambao wamefiwa na wapendwa wao. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, Amen.

3) **Mheshimiwa Spika**, ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kushiriki katika Mkutano wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, kwa namna ya kipekee naomba nitumie fursa hii kumpongeza Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe.

Samia Suluhu Hassan Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na viongozi wote wa Serikali kwa mafanikio makubwa yanayoendelea kupatikana katika Serikali ya Awamu ya Tano. Kwa kasi hii tunayokwenda nayo ikichagizwa na kauli mbiu ya “**Hapa Kazi Tu**”, nina hakika tutafikia dhamira ya Tanzania ya viwanda. Aidha, nawapongeza kwa dhati Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Mhe. Balozi Seif Ali Idd, Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Mbunge wa Jimbo la Kitope kwa mafanikio makubwa yanayoendelea kupatikana chini ya uongozi wao imara.

- 4) **Mheshimiwa Spika**, naomba nitumie fursa hii pia kukupongeza wewe binafsi na Naibu Spika Mhe. Dkt. Tulia Ackson Mwansasu (Mb.) kwa jinsi mnavyosimamia shughuli za Bunge hili Tukufu kwa umakini wa hali ya juu. Vilevile, ninawapongeza Wenyeviti wa Bunge lako Tukufu Mhe. Andrew John Chenge (Mb.), Mhe. Najma Murtaza Giga (Mb.) na Mhe. Azzan Mussa Zungu (Mb.) ambao kwa nyakati tofauti wamekuwa wakiongoza shughuli za Bunge kwa

ufanisi. Mwenyezi Mungu aendelee kuwaongoza na kuwapa nguvu, afya njema na hekima ili muendelee kutimiza jukumu hili.

5) **Mheshimiwa Spika**, napenda kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mhe. Juma Ali Juma kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Dimani. Aidha, ninawapongeza Wabunge wapya walioteuliwa kuingia katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambao ni Mhe. Profesa Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi, ambaye pia ameteuliwa kuwa Waziri wa Katiba na Sheria; Mhe. Alhaji Abdallah Majura Bulembo, Mhe. Anne Kilango Malecela, Mhe. Salma Rashid Kikwete, Mhe. Mchungaji Dkt. Getrude Pangalile Rwakatare na Mhe. Catherine Nyakao Ruge. Ninawatakia kila la kheri katika utekelezaji wa majukumu yenu.

6) **Mheshimiwa Spika**, naomba kutumia fursa hii kumpongeza Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.) Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hotuba yake ambayo imeelezea utekelezaji wa malengo ya Serikali katika mwaka wa fedha 2016/17 na mwelekeo wa utendaji wa sekta mbalimbali pamoja na kazi za Serikali

zitakazotekelezwa katika mwaka wa fedha 2017/18. Wizara yangu itayafanyia kazi yale yote yanayoihusu sekta ya ardhi ili kuhakikisha kwamba malengo ya Serikali ya Awamu ya Tano yanafikiwa.

- 7) **Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya kipekee natoa shukrani zangu za dhati kwa wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii chini ya Mwenyekiti wake Mhe. Mhandisi Atashasta Justus Nditiye (Mb.) akisaidiwa na Makamu Mwenyekiti Mhe. Kemirembe Rose Julius Lwota (Mb.) pamoja na Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano mkubwa na ushauri wao ambao unaiwezesha Wizara kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha, nawashukuru kwa uchambuzi makini walioufanya na ushauri walioutoa wakati wa kupitia taarifa ya utekelezaji wa mpango na bajeti ya mwaka wa fedha 2016/17 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu Na. **48**, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Fungu Na. **03**, Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi kwa mwaka wa fedha 2017/18. Ninawashukuru kwa maoni na ushauri waliotoa wakati Kamati ilipotembelea miradi na taasisi zinazosimamiwa na Wizara na kujadili masuala

mbalimbali yanayohusu sekta ya ardhi. Ushauri wao utaendelea kuzingatiwa wakati wote wa utekelezaji wa majukumu ya Wizara yangu.

- 8) ***Mheshimiwa Spika***, natoa shukrani za pekee kwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mhe. Dkt. Angeline Sylvester Lubala Mabula (Mb.) kwa ushirikiano mkubwa na ushauri anaonipa wakati wote wa utekelezaji wa majukumu yangu. Pia, ninawashukuru Katibu Mkuu Dkt. Yamungu Kayandabila; Naibu Katibu Mkuu, Dkt. Moses Kusiluka; Wakuu wa Idara na Vitengo, Shirika la Nyumba la Taifa, Wakala na Taasisi zilizo chini ya Wizara yangu pamoja na watumishi wote wa sekta ya ardhi katika ngazi zote kwa kuendelea kutekeleza majukumu yao. **Nawakumbusha watumishi wote wa sekta ya ardhi nchini kutimiza majukumu yao kwa weledi na kwa kuzingatia sera, sheria, kanuni, taratibu na miongozo iliyopo na itakayokuwa inatolewa ili kuboresha utoaji wa huduma za sekta ya ardhi.**

- 9) ***Mheshimiwa Spika***, baada ya maelezo ya utangulizi, naomba sasa nieleze kwa kifupi utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2016/17, na makadirio

ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2017/18. Takwimu za taarifa ya utekelezaji wa bajeti zilizopo katika hotuba hii zinaishia tarehe 15 Mei, 2017.

B: MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2016/17 NA MALENGO YA MWAKA WA FEDHA 2017/18

- 10) *Mheshimiwa Spika*, katika kutekeleza majukumu, Wizara imeendelea kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Mpango wa II wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17-2020/21); Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2015-2020; Mpango Mkakati wa Wizara (2012/13-2016/17); Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995; Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000 pamoja na miongozo mbalimbali ya Serikali.

Mapato na Matumizi ya Fedha: Fungu 48 (Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi)

Ukusanyaji wa Mapato

- 11) *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2016/17, Wizara ilipanga kukusanya Shilingi bilioni **111.77** kutokana na vyanzo vya mapato

yanayotokana na kodi, ada na tozo mbalimbali za ardhi. Hadi tarehe 15 Mei, 2017, Wizara ilikuwa imekusanya Shilingi bilioni **80.52** sawa na asilimia **72** ya lengo. Aidha, katika mwaka wa fedha 2015/16 Wizara ilikusanya Shilingi bilioni **74.71**, sawa na asilimia **107** ya lengo la kukusanya Shilingi bilioni **70.00**. Ni matarajio yetu kwamba hadi kufikia Juni 2017, lengo la kukusanya Shilingi bilioni **111.77** litafikiwa kwa kutekeleza mpango mkakati wa Wizara. **Jedwali Na. 1** linaonesha hali ya makusanyo. **Nachukua fursa hii kuwapongeza wamiliki wa ardhi waliolipa kodi ya pango la ardhi kwa wakati. Aidha, nawataka wamiliki wa ardhi wote ambao hawajalipa kodi hiyo wahakikishe wanalipa kabla ya tarehe 30 Juni, 2017. Serikali itaendelea kuwachukulia hatua kali wamiliki wote ambao hawalipi kodi kwa wakati ikiwa ni pamoja na kuwafutia miliki, kuwafikisha mahakamani, na kukamata na kuuza mali zao.**

- 12) ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2016/17 Wizara iliahidi kuhuisha viwango vya kodi ya ardhi kwa mashamba ya biashara yaliyoko nje ya miji yaliyomilikishwa chini ya Sheria ya Ardhi Na. 4 ya mwaka 1999. Baada ya kupitia viwango hivyo, Serikali inakusudia

kuongeza viwango vya pango la ardhi kutoka Shilingi **400/=** hadi Shilingi **800/=** kwa ekari kwa mwaka kuanzia Julai, 2017 kwa mashamba ya biashara yaliyopimwa na kumilikishwa nje ya miji. Kiwango kinachotozwa sasa cha Shilingi **400/=** kwa ekari moja bado ni kidogo sana ikilinganishwa na thamani pamoja na uwezo wa uzalishaji wa ardhi husika.

- 13) **Mheshimiwa Spika**, ili kuwawezesha wananchi wengi kumiliki maeneo yao kwa gharama nafuu pamoja na kupanua wigo wa walipaji wa kodi ya pango la ardhi, Serikali inatarajia kupunguza tozo ya mbele (*premium*) kutoka asilimia **7.5** hadi asilimia **2.5** ya thamani ya ardhi kuanzia Julai, 2017. Ada hii hutozwa mara moja tu wakati wa umilikishaji ardhi kwa mujibu wa fungu la 31 la Sheria ya Ardhi Na. 4 ya mwaka 1999. Kupunguzwa kwa kiwango cha tozo ya mbele kutavutia wananchi wenye maeneo ya ardhi kujitokeza kwa wingi zaidi kupimiwa na kumilikishwa ardhi yao. **Natoa rai kwa wananchi wote kutumia fursa hii ya punguzo la tozo ya mbele kupima na kumilikishwa maeneo yao na kulipa kodi.**

14) **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2017/18, Wizara inatarajia kukusanya Shilingi bilioni **112.05** kutokana na shughuli za sekta ya ardhi. Mapato hayo yatatokana na vyanzo mbalimbali vya kodi ya pango la ardhi, ada na tozo mbalimbali za ardhi. Lengo hili litafikiwa kwa kutekeleza mikakati ifuatayo:-

- i) Kuongeza kasi ya kurasimisha maeneo yasiyopangwa mijini;
- ii) Kuimarisha mifumo iliyopo ya utunzaji wa kumbukumbu za ardhi;
- iii) Kuendelea kupima maeneo mapya pamoja na kukamilisha upimaji na umilikishaji wa viwanja katika maeneo ambayo upimaji wake haujakamilika;
- iv) Kuhimiza wamiliki wote wa ardhi nchini kulipa kodi ya ardhi kwa mujibu wa sheria na kuwachukulia hatua wadaiwa sugu ikiwemo kuwafikisha mahakamani;
- v) Kushirikisha sekta binafsi katika upangaji na upimaji wa ardhi ili kuongeza idadi ya viwanja na hivyo kuongeza wigo wa mapato;
- vi) Kuanza kutoza kodi ya pango la ardhi kwenye maeneo ambayo hayajapimwa mijini; na
- vii) Kurahisisha ulipaji wa kodi ya pango la ardhi kwa kuwawezesha wananchi kufanya

malipo kwa kutumia mitandao ya simu na kuongeza idadi ya benki za kukusanya kodi.

Matumizi

- 15) **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2016/17, Wizara iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni **70.49** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni **16.34** zilitengwa kwa ajili ya mishahara; shilingi bilioni **28.85** kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi bilioni **25.30** kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2017, Wizara ilikuwa imepokea na kutumia jumla ya shilingi bilioni **34.95** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo, sawa na asilimia **50** ya lengo la mwaka. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni **13.21** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo ambapo shilingi bilioni **2.28** zilitolewa kwa halmashauri mbalimbali kwa ajili ya kuendeleza shughuli za sekta ya ardhi, shilingi bilioni **14.11** ni fedha za mishahara na shilingi bilioni **7.63** ni fedha za miradi ya maendeleo (**Jedwali Na. 2**).

Mapato na Matumizi ya Fedha: Fungu 03 (Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi)

Ukusanyaji wa Mapato

- 16) **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2016/17, Tume ilikuwa na lengo la kukusanya shilingi milioni **775.25** kutoka kwenye vyanzo mbalimbali ambavyo ni: kodi ya pango la nyumba za Tabora na mauzo ya nyaraka za zabuni. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2017, Tume ilikuwa imekusanya shilingi milioni **531.66** sawa na asilimia **69** ya lengo.

Matumizi

- 17) **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2016/17, Tume iliidhinishiwa Shilingi bilioni **1.75** kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, Shilingi milioni **845.28** zilitengwa kwa ajili ya mishahara na Shilingi milioni **901.62** kwa ajili ya matumizi mengineyo. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2017, Tume ilipokea jumla ya Shilingi bilioni **1.16** sawa na asilimia **66** ya fedha iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, Shilingi milioni **494.04** ni matumizi mengineyo sawa na asilimia **55** ya fedha zilizoidhinishwa na Shilingi milioni **665.47** ni fedha za mishahara.

HUDUMA ZA MAENDELEO YA ARDHI

18) ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2016/17, Wizara yangu iliendelea kutoa huduma za ardhi kwa wananchi. Huduma hizo ni pamoja na utoaji wa hatimiliki za ardhi; hati za hakimiliki za kimila; uthamini; usajili wa hati, nyaraka na miamala ya ardhi; kushughulikia migogoro ya ardhi kiutawala na uhakiki wa milki. Pamoja na shughuli hizi, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri nchini imeendelea kuhimiza wananchi kuzingatia masharti ya umiliki wa ardhi na kuchukua hatua dhidi ya ukiukwaji wa masharti hayo, mathalan; kutoendeleza ardhi, kuendeleza ardhi kinyume na masharti na kutolipa kodi ya pango la ardhi. Aidha, Wizara iliendelea kuimarisha kumbukumbu za ardhi na kutoa ushauri kuhusu masuala mbalimbali ya ardhi nchini.

Usimamizi wa Ardhi

19) ***Mheshimiwa Spika***, usimamizi wa ardhi nchini ni suala mtambuka kwa kuwa linahusisha mamlaka mbalimbali zikiwemo Halmashauri za Vijiji, Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa, Majiji na Wizara yangu. Pamoja na uwepo wa mamlaka hizi, Wizara imeendelea kupokea hoja

na malalamiko mbalimbali yanayohusiana na ardhi kutoka kwa wananchi ambayo kimsingi yangeweza kushughulikiwa katika ngazi za vijiji au halmashauri husika. **Napenda kuwakumbusha wananchi kutumia ofisi za Halmashauri kwa ajili ya kutatua kero zao kabla ya kuwasilisha kero hizo katika ngazi ya Wizara.**

Kuimarisha Huduma katika Ofisi za Ardhi za Kanda

20) ***Mheshimiwa Spika***, katika kuboresha utoaji huduma, Wizara imeendelea kuimarisha Ofisi za Ardhi za Kanda kwa kupeleka wataalam wa kada mbalimbali. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2017, Wizara imepeleka watumishi wa kada ya wapima ardhi na wasajili katika ofisi ya kanda ya Ziwa (Mwanza), kanda ya Kusini (Mtwara) na Kanda ya Magharibi (Tabora). Aidha, vitendea kazi mbalimbali ikiwa ni pamoja na magari mapya nane (8) vimepelekwa katika kanda zote nane (8). Katika mwaka wa fedha 2017/18, watumishi wa kada ya maafisa ardhi, wasajili wa hati, wathamini, wapima ardhi na maafisa mipangomiji watapelekwa katika ofisi za kanda zote. Lengo la hatua hii ni kuwawezesha wananchi kupata huduma mbalimbali za ardhi katika kanda

badala ya kuzifuata huduma hizo Makao Makuu ya Wizara.

- 21) **Mheshimiwa Spika**, katika kusogeza huduma za ardhi karibu zaidi na wananchi, Wizara vilevile imeboresha muundo wa ofisi za kanda kwa kuanzisha kanda mpya ya Simiyu, kupunguza na kuongeza mikoa katika baadhi ya kanda. Kuanzia Julai, 2017 Ofisi za Ardhi za Kanda zitakuwa zikihudumia mikoa kama ifuatavyo; **Kanda ya Dar es Salaam** (Dar es Salaam) itahudumia mikoa ya Dar es Salaam na Pwani; **Kanda ya Nyanda za Juu Kusini** (Mbeya) itahudumia mikoa ya Mbeya, Njombe, Rukwa na Songwe; **Kanda ya Kati** (Dodoma) itahudumia mikoa ya Dodoma, Singida, Iringa na Morogoro; **Kanda ya Kaskazini** (Arusha) itahudumia mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Tanga na Manyara; **Kanda ya Ziwa** (Mwanza) itahudumia mikoa ya Mwanza, Geita na Kagera; **Kanda ya Magharibi** (Tabora) itahudumia mikoa ya Tabora, Kigoma na Katavi; **Kanda ya Kusini** (Mtwara) itahudumia mikoa ya Mtwara, Lindi na Ruvuma na **Kanda ya Simiyu** (Bariadi) itakayohudumia mikoa ya Simiyu, Shinyanga na Mara.

Kuvunjwa kwa Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu (CDA)

22) **Mheshimiwa Spika**, kufuatia uamuzi wa Serikali wa kuvunja CDA, kufutwa kwa hatimiliki ya ardhi ya CDA na kuhamishia shughuli zake katika Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma, kuanzia sasa wananchi watamilikishwa ardhi kwa kupewa hatimiliki za muda wa miaka 99. Wamiliki waliokuwa na mikataba ya pango la ardhi (*ground lease*) iliyotolewa na CDA watahakikiwa na kumilikishwa upya kwa kupewa hatimiliki ya miaka 99 bila kulipa tena gharama za umilikishaji. Hata hivyo, kabla ya kumilikishwa watapaswa kulipa malimbikizo ya kodi ya pango la ardhi. Aidha, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa haki za wananchi na taasisi za fedha zinazohusiana na mikataba ya pango iliyotumika kama dhamana kupata mikopo na miamala mingine iliyokuwa haijakamilika hazitaathirika na mabadiliko haya.

23) **Mheshimiwa Spika**, kuanzia sasa wananchi wote wanaohitaji huduma za ardhi watapata huduma hizo kupitia Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma na hati zitatolewa na Ofisi ya Kanda ya Kati. Kufuatia kuongezeka kwa majukumu

katika kanda hiyo, Wizara itaongeza vitendea kazi na wataalam wa kada ya maafisa ardhi, wasajili wa hati, wathamini, wapima ardhi na maafisa mipangomiji.

Utoaji Milki za Ardhi

24) **Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri na sekta binafsi imeendelea kuhakikisha kuwa kila kipande cha ardhi nchini kinapangwa, kupimwa na kumilikishwa. Halmashauri mbalimbali kwa kushirikiana na sekta binafsi zimekamilisha miradi ya upimaji wa viwanja katika miji mbalimbali nchini (**Jedwali Na. 3**). Katika mwaka wa fedha 2017/18 Wizara yangu itaendelea kuhimiza ushiriki wa sekta binafsi katika kupanga na kupima ardhi ili kuongeza kasi ya utoaji wa milki za ardhi nchini. Ushiriki wa sekta binafsi utaongeza fursa za ajira, kuongeza mapato ya Serikali yatokanayo na kodi ya pango la ardhi na kukuza pato la Taifa.

25) **Mheshimiwa Spika**, katika utekelezaji wa Sera na Sheria za Ardhi, Wizara inaratibu utoaji wa vyeti vya ardhi ya vijiji, hati za hakimiliki za kimila, hatimiliki za ardhi, kutoa elimu kwa wananchi kwa kushirikiana na wadau

mbalimbali na kutatua migogoro kwa njia za kiutawala. Katika mwaka wa fedha 2016/17, Wizara iliahidi kuandaa hatimiliki za ardhi **400,000** na kutoa hati za hakimiliki za kimila **57,000**. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2017 Wizara imetoa hatimiliki za ardhi **33,979** na imeratibu uandaaji wa hati za hakimiliki za kimila **35,002**. Aidha, Wizara imeandaa vyeti vya ardhi ya kijiji **505 (Jedwali Na. 4)**. Napenda kutambua ushiriki wa wadau mbalimbali kwa mchango wao katika kuwezesha utoaji wa vyeti vya ardhi ya kijiji na hati za hakimiliki za kimila. Baadhi ya wadau hao ni; MKURABITA, USAID, DFID, DANIDA na SIDA. Wengine ni *Oxfam International Tanzania, Care International Tanzania, Ujamaa Community Resource Team, African Wildlife Foundation, Eco Village Adaptation to Climate Change in Central Tanzania, Tanzania Natural Resource Forum, SNV Netherlands Development Organization* na HakiArdhi.

- 26) **Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka wa fedha 2017/18, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri nchini itaandaa hatimiliki za ardhi **400,000**, vyeti vya ardhi ya vijiji **1,000** na kutoa hati za hakimiliki za kimila **57,000**. Aidha, ili kuwawezesha wananchi wengi kupata hatimiliki

za ardhi, Wizara inakusudia kupunguza tozo ya mbele ambayo hutozwa wakati wa kumilikisha ardhi kutoka asilimia **7.5** mpaka asilimia **2.5** ya thamani ya ardhi. **Natoa rai kwa Halmashauri zote nchini kuhakikisha kuwa zinamilikisha viwanja vyote vilivyopimwa na kuandaa Hati ili wananchi waweze kuwa na miliki salama.**

Kamati za Ugawaji Ardhi

27) **Mheshimiwa Spika**, Wizara inalo jukumu la kuteua wajumbe wa Kamati za Ugawaji Ardhi katika Halmashauri baada ya kupokea mapendekezo kutoka katika halmashauri husika. Kamati hizi ni muhimu katika kusimamia ugawaji wa ardhi nchini ili kuepuka ugawaji ardhi usiozingatia sheria ambao wakati mwingine husababisha migogoro ya ardhi. Katika mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara yangu imeidhinisha uteuzi wa Kamati za Kugawa Ardhi katika Halmashauri **19**. Halmashauri zilizohusika katika uteuzi ni Jiji la Arusha, Manispaa ya Moshi, Manispaa ya Tabora, Manispaa ya Kigoma, Mji wa Ifakara, Wilaya ya Arusha, Simanjiro, Kongwa, Mpanda, Kasulu, Mwanga, Siha, Chalinze, Mafia, Mkalama, Urambo, Bunda, Buhigwe na Itigi. Uteuzi huu umefanya jumla ya Halmashauri **102** kuwa na Kamati za Kugawa Ardhi, kati

ya Halmashauri 184 zinazotakiwa kuwa na kamati hizo (**Jedwali Na. 5**). **Nazikumbusha Halmashauri ambazo bado hazina Kamati za Ugawaji wa Ardhi kuwasilisha mapendekezo ya wajumbe wa Kamati hizi kwa ajili ya uteuzi.**

- 28) ***Mheshimiwa Spika***, Wizara yangu pia inasimamia shughuli za Kamati ya Taifa ya Ugawaji Ardhi ambayo, pamoja na majukumu mengine, huidhinisha maombi ya ardhi kwa ajili ya uwekezaji. Katika mwaka wa fedha 2016/17, Kamati hii ilipitia maombi **46** na kuidhinisha ugawaji wa viwanja **40** na mashamba **6** ya uwekezaji kwa ajili ya matumizi ya kilimo, biashara, hoteli, makazi ya zaidi ya familia moja na viwanda (**Jedwali Na. 6**). **Natoa rai kwa Halmashauri zote nchini zishirikiane na Kituo cha Uwekezaji Tanzania ili kuharakisha maombi ya wawekezaji.**

Uhakiki wa Viwanja na Mashamba

29) **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2016/17, Wizara iliendelea kuhakiki viwanja na mashamba nchini ili kubaini ukiukwaji wa masharti ya umiliki. Kutokana na uhakiki uliofanyika, Wizara imechukua hatua ya kubatilisha milki za viwanja **227** na mashamba **17** kutokana na ukiukwaji wa masharti. Viwanja na mashamba haya yapo katika mikoa ya Dar es Salaam, Mbeya, Mwanza, Iringa, Kagera na Morogoro.

30) **Mheshimiwa Spika**, vilevile, Wizara imeshughulikia maombi ya kuhawilisha mashamba yenye ukubwa wa jumla ya hekta **25,259** yaliyopo katika wilaya ya Rufiji mkoani Pwani ili kuwezesha uwekezaji wa kilimo cha miwa kwa ajili ya uzalishaji wa sukari. Ardhi ya mashamba yaliyobatilihwa na yaliyohawilishwa itasaidia kupatikana kwa ardhi ya kutosha kwa ajili ya uwekezaji mkubwa utakaowezesha uzalishaji wa malighafi za viwanda. Aidha, Wizara yangu imepanga na kupima ardhi yenye ukubwa wa hekta **433** katika eneo la Pembamnazi lililopo Manispaa ya Kigamboni kwa ajili ya matumizi ya viwanda. Katika mwaka wa fedha 2017/18, Wizara yangu itaendelea kuongeza hazina ya

ardhi kwa ajili ya matumizi mbalimbali ikiwemo uwekezaji mkubwa katika sekta ya viwanda ili kufanikisha azma ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kuwa na Tanzania ya viwanda.

Usimamizi wa Ardhi ya Uwekezaji

31) **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2016/17, Wizara iliahidi kufuatilia uwekezaji na uendelezaji wa mashamba na viwanja na kuweka taarifa hizo kwenye kanzidata. Hatua hii inalenga kuwa na kumbukumbu sahihi za ardhi ya uwekezaji iliyoendelezwa na kubaini iwapo inatumika kwa malengo yaliyokusudiwa. Mpaka sasa Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri imefanya ukaguzi wa mashamba ya uwekezaji **121** yenye ukubwa wa ekari **552,139.21** yaliyopo katika mikoa ya Tanga, Morogoro, Pwani, Njombe na Kagera na kuingiza taarifa zake katika kanzidata ya Wizara. Kati ya mashamba haya, **63** yameendelezwa na **58** yametelekezwa. Kwa mashamba ambayo hayajaendelezwa, hatua za kisheria zinaendelea kuchukuliwa. Katika mwaka wa fedha 2017/18, Wizara yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Takwimu itafanya uhakiki wa mashamba ya uwekezaji nchini.

Utatuzi na Udhhibiti wa Migogoro ya Matumizi ya Ardhi

32) **Mheshimiwa Spika**, katika Hotuba ya bajeti ya Wizara ya mwaka wa fedha 2016/17 suala la migogoro ya ardhi liligusa hisia za Waheshimiwa Wabunge wengi na waliitaka Serikali kuwa na mkakati maalum wa kushughulikia suala hili. Kwa kutambua kuwa migogoro ya matumizi ya ardhi ni suala mtambuka, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Ofisi ya Taifa ya Takwimu iliunda kamati ya kisekta ili kubaini aina na vyanzo vya migogoro na kupendekeza namna bora ya kutatua migogoro hiyo. Baada ya kupokea taarifa ya kamati, Serikali inafanya uchambuzi utakaowezesha kuchukua hatua ili kutatua migogoro hiyo. Aidha, migogoro mingine ilitatuliwa kupitia mikutano niliyofanya na wananchi katika ziara nilizofanya sehemu mbalimbali nchini. Kadhalika migogoro mingine ilitatuliwa kwa kushughulikia malalamiko yaliyowasilishwa Wizarani na kwenye ofisi za kanda.

Mfuko wa Fidia ya Ardhi

33) **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2016/17, nililiarifu Bunge lako Tukufu kwamba Wizara inakamilisha uundaji wa Bodi ya Mfuko wa Fidia kwa mujibu wa Kifungu Na. 173 cha Sheria ya Ardhi (Sura 113) na Kanuni zinazosimamia Mfuko wa Fidia za mwaka 2001. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Bodi hii imeshaundwa rasmi baada ya Mwenyekiti na wajumbe wake kuteuliwa. Bodi ya Mfuko wa Fidia itaratibu shughuli zote za ulipaji wa fidia nchini zitakazofanywa na Wizara, Idara za Serikali zinazojitegemea, Wakala, Mikoa na Halmashauri ili kuondoa kero kwa wananchi ikiwemo kuchelewa kulipwa fidia, kupunjwa au kutolipwa fidia. Wizara yangu itaandaa na kusambaza mwongozo wa namna ya shughuli za mfuko wa fidia zitakavyofanyika.

Programu ya Kuwezesha Umilikishaji Ardhi

34) **Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu inaendelea na utekelezaji wa Programu ya Kuwezesha Umilikishaji Ardhi (**Land Tenure Support Programme**) katika Wilaya za Kilombero, Ulanga na Malinyi mkoani Morogoro chini ya ufadhili wa Serikali ya nchi za Uingereza, Sweden na Denmark kupitia Mashirika yao ya Maendeleo ya

DFID, SIDA na DANIDA. Katika mwaka wa fedha 2016/17, Wizara yangu iliahidi kuandaa Hati za Hakimiliki za Kimila **50,000** katika vijiji **40** vya eneo la mradi na kujenga masjala za ardhi katika vijiji hivyo. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2017 Hati za Hakimiliki za Kimila **11,403** zimeandaliwa katika vijiji **7** vya Wilaya za Kilombero (hati **8,303** katika vijiji **4**) na Ulanga (hati **3,100** katika vijiji **3**).

- 35) **Mheshimiwa Spika**, katika utekelezaji wa Programu hii Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Vijiji **18** imeandaliwa katika Wilaya za Kilombero (**8**) na Ulanga (**10**). Aidha, alama za msingi za upimaji (*control points*) **54** zimesimikwa ili kuwezesha upimaji wa mipaka ya vijiji na hatimaye vipande vya ardhi ambavyo vitaandaliwa hati za hakimiliki za kimila. Alama hizo zimesimikwa katika Wilaya za Ulanga (**16**), Kilombero (**26**), Malinyi (**10**) na Mufindi (**2**). Vilevile, mipaka ya vijiji **52** imepimwa katika wilaya za Kilombero (**30**), Ulanga (**19**) na Malinyi (**3**). Kutokana na upimaji huo jumla ya vyeti vya ardhi ya vijiji **45** vimeandaliwa na kutolewa. Vilevile, ili kuwa na mazingira bora ya kuhifadhi kumbukumbu za ardhi, Wizara imehamasisha ujenzi na ukarabati wa masjala za ardhi na ofisi za vijiji katika vijiji

61 katika wilaya za Kilombero (vijiji **28**), Ulanga (vijiji **18**) na Malinyi (vijiji **15**).

36) **Mheshimiwa Spika**, ili matokeo ya utekelezaji wa Programu yawe endelevu hususan baada ya Programu kukamilika katika Wilaya za Kilombero, Ulanga na Malinyi, Wizara imekuwa ikishirikiana kikamilifu na Halmashauri za Wilaya tajwa pamoja na vijiji katika utekelezaji wa Programu. Aidha, wataalam wa Halmashauri za Wilaya pamoja na Kamati za Usimamizi wa Matumizi ya Ardhi ya Kijiji na Kamati za Uhakiki za Vijiji wamejengewa uwezo katika kuandaa Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Vijiji na kupima vipande vya ardhi ili kutoa Hati za Hakimiliki za Kimila.

37) **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2017/18 Wizara kupitia Programu ya Kuwezesha Umilikishaji Ardhi imepanga kufanya uhakiki wa vipande vya ardhi **80,000** na kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji **37**; kujenga ofisi za ardhi katika wilaya za Kilombero (**1**), Ulanga (**1**) na Malinyi (**1**); na kuandaa vyeti vya ardhi vya vijiji **15** katika wilaya za Kilombero, Ulanga na Malinyi.

Usajili wa Hati Miliki na Nyaraka za Kisheria

38) **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/17 Wizara yangu ilipanga kusajili Hatimiliki na Nyaraka za Kisheria **450,500** kati ya hizo **400,000** ni Hatimiliki, **2,500** Hati za kumiliki sehemu ya jengo na Nyaraka za Kisheria **48,000**. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2017 Hatimiliki pamoja na Nyaraka za Kisheria **79,117** zimesajiliwa. Kati ya hizo Hatimiliki ni **32,178** na nyaraka nyingine za kisheria **46,939**. Nyaraka **29,304** zimesajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Ardhi (Sura 334) na Hati za Umiliki wa Sehemu ya Jengo **1,343** zimesajiliwa chini ya Sheria ya Umiliki wa Sehemu ya Jengo (Sura 416) (**Jedwali 7A**). Aidha, Nyaraka za Kisheria zipatazo **16,975** zimesajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Nyaraka (Sura 117) (**Jedwali 7B**) na nyaraka **660** zilisajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Rehani ya Mali zinazohamishika (Sura 210) (**Jedwali 7C**).

39) **Mheshimiwa Spika**, wananchi wanahamasishwa kupima maeneo yao na kupata hatimiliki. Hati hizi zina umuhimu mkubwa ikiwemo kuwahakikishia usalama wa miliki zao na pia zinaweza kutumika kama dhamana za mikopo katika taasisi za fedha. **Ninawahimiza wananchi kufanya uhakiki kwenye Ofisi ya**

Msajili wa Hati kila wanapokusudia kufanya miamala inayohusu ardhi ili kuepuka utapeli.

- 40) **Mheshimiwa Spika**, nachukua fursa hii kuwahamasisha wananchi kuona umuhimu wa kusajili nyaraka mbalimbali za kisheria kama vile nyaraka zinazotoa mamlaka, mabadiliko ya majina, wosia na mikataba ya mikopo. Nyaraka hizi husajiliwa katika Ofisi za Msajili wa Hati kwenye kanda husika. Hatua hii itasaidia kuhakikisha usalama wa nyaraka hizo na kurahisisha upatikanaji wa nyaraka husika pindi zinapohitajika kwa matumizi mbalimbali. Katika mwaka wa fedha 2017/18, Wizara inakusudia kusajili hatimiliki na nyaraka za kisheria **453,000**. Kati ya hizi, hati za kumiliki ardhi ni **400,000**, hati za kumiliki sehemu ya jengo **3,000** na nyaraka za kisheria **50,000**.

Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA)

- 41) **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2016/17, Serikali iliahidi kuanza ujenzi wa Mfumo Unganishi wa Kuhifadhi Kumbukumbu za Ardhi (*Integrated Land Management Information System-ILMIS*). Katika kutekeleza ahadi hii, Serikali imeingia mkataba na mkandarasi (IGN FI) wa kujenga Mfumo huo. Mkataba huo

ulisainiwa tarehe 5 Julai, 2016. Kazi ya ujenzi wa Mfumo ilizinduliwa rasmi tarehe 26 Agosti, 2016 na mkandarasi tayari ameanza kazi. Sambamba na ujenzi wa mfumo huu, Serikali imekamilisha ukarabati wa jengo la Kituo cha Taifa cha Taarifa za Ardhi (NLIC) na ufungaji wa baadhi ya vifaa umekamilika. Kukamilika kwa mradi huu kutaboresha utunzaji wa kumbukumbu na nyaraka za ardhi, kurahisisha utendaji kazi, kuharakisha huduma za utoaji wa milki na kuongeza mapato ya Serikali. Katika mwaka wa fedha 2017/18, Wizara itaanza kutoa hati za kielektroniki katika Manispaa za Kinondoni na Ubungo.

- 42) **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2016/17, Wizara iliahidi kukamilisha usimikaji wa Mfumo wa Kielektroniki wa Kuhifadhi Kumbukumbu na Kukadiria Kodi ya Ardhi (*Land Rent Management System-LRMS*) katika Halmashauri 17 zilizobaki kati ya 184. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa kazi hii imekamilika katika Halmashauri 10 na inaendelea katika Halmashauri saba (7) zilizobaki ambazo ni Buhigwe, Nanyamba, Momba, Madaba, Mbogwe, Buchosa na Mpimbwe. Katika mwaka wa fedha 2017/18 Wizara itaendelea kuboresha Mfumo wa

Ukusanyaji wa Kodi ya Pango la Ardhi ili uweze kuongeza ufanisi katika makusanyo ya kodi, umilikishaji ardhi na usajili wa hati.

Uthamini wa Mali

- 43) **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2016/17, Wizara iliahidi kuandaa na kuidhinisha taarifa **32,500** za uthamini wa kawaida na fidia kwa matumizi mbalimbali. Hadi tarehe 15 Mei, 2017 Wizara iliidhinisha taarifa za uthamini **8,725** ambapo taarifa **97** ni uthamini wa fidia na **8,628** ni uthamini wa mali kwa madhumuni mbalimbali kama vile rehani, dhamana mahakamani, bima, mirathi na mgawanyo wa mali kwa wanandoa (**Jedwali Na. 8A & 8B**). Taarifa hizi ni kwa ajili ya matumizi ya utozaji ada na ushuru wa Serikali unaotokana na uthamini. Aidha, Wizara ilishiriki kufanya uthamini wa fidia katika baadhi ya miradi ya kitaifa ikiwemo upanuzi wa viwanja vya ndege Dodoma, Kigoma na Chato; upanuzi wa eneo la Ikulu - Chamwino na utwaaji wa eneo la mradi wa gesi asilia eneo la Likong'o mkoani Lindi. Katika mwaka wa fedha 2017/18, Wizara inatarajia kuandaa na kuidhinisha taarifa **35,000** za uthamini. **Napenda kuutarifu umma wa Watanzania kwamba, kufuatia kuanza kutumika kwa Sheria ya Uthamini na Usajili**

wa Wathamini Na. 7 ya mwaka 2016, taarifa zote za uthamini zinapaswa kuidhinishwa na Mthamini Mkuu wa Serikali.

Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya

44) **Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu kwa mujibu wa Sheria ya Mahakama za Ardhi Na. 2 ya mwaka 2002 ina jukumu la kuanzisha na kusimamia Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya kwa lengo la kupokea, kusikiliza na kutatua migogoro ya ardhi nchini. Katika mwaka wa fedha 2016/17 Wizara yangu imefungua Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya katika wilaya za Kilindi, Lushoto na Kiteto hivyo kufanya jumla ya mabaraza yanayofanya kazi kuwa **53** kwa nchi nzima. Katika mwaka wa fedha 2016/17 Wizara iliahidi kushughulikia mashauri **13,590** yaliyokuwepo na ambayo yangefunguliwa. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2017 jumla ya mashauri **40,135** yalishughulikiwa ambapo kati ya hayo mashauri **18,571** yaliamuliwa (**Jedwali Na.9**). Katika mwaka wa fedha 2017/18 Wizara itaendelea kushughulikia mashauri yaliyobaki na yatakayofunguliwa.

45) **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2016/17 Wizara iliahidi kuendelea kuboresha utendaji kazi wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya kwa kuongeza idadi ya ofisi za Mabaraza na kuyapatia vitendea kazi muhimu. Aidha, Wizara iliahidi kuanzisha Mabaraza mapya katika Wilaya tano (5) ambazo ni Lushoto, Bagamoyo, Kiteto, Kasulu na Kibondo. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Mabaraza ya Wilaya za Kilindi, Kiteto na Lushoto tayari yameanza kufanya kazi. Kwa Mabaraza ya Bagamoyo, Kasulu na Kibondo majengo yalikiwishapatikana, tathmini ya gharama za ukarabati zimeshafanyika na ukarabati ukikamilika mabaraza hayo yataanza kufanya kazi. Katika mwaka wa fedha 2017/18 Wizara yangu inatarajia kuzindua Mabaraza ya Wilaya za Kongwa, Mpwapwa na Urambo. Hadi sasa Mabaraza **39** bado hayajazinduliwa kutokana na ukosefu wa majengo na samani. **Natoa wito kwa Halmashauri za Wilaya kutoa majengo yanayoweza kutumika kwa shughuli za Mabaraza bila kuhitaji gharama kubwa za ukarabati.**

HUDUMA ZA UPIMAJI NA RAMANI

Huduma za Ramani

46) **Mheshimiwa Spika**, mojawapo ya majukumu ya Wizara yangu ni kutayarisha ramani za msingi ambazo ni chanzo muhimu cha taarifa zinazohitajika katika kubuni na kutayarisha mipango ya maendeleo kwa sekta mbalimbali. Katika mwaka wa fedha 2016/17, Wizara iliahidi kuendelea kuhakiki na kuandaa ramani za mipaka ya wilaya mpya kwa mujibu wa Matangazo ya Serikali yaliyoanzisha wilaya hizo. Wizara imekamilisha uhakiki na uandaaji wa ramani za wilaya mpya tano (5) ambazo ni Nyang'hwale, Geita, Bukombe, Mbogwe na Chato. Katika mwaka wa fedha 2017/18, Wizara itahuisha ramani za msingi za uwiano wa 1:50,000 kwenye miji 50.

47) **Mheshimiwa Spika**, Wizara imebaini kuwepo kwa baadhi ya taasisi binafsi zinazojihusisha na uandaaji wa ramani na kuziuzua bila idhini ya Wizara yangu, jambo ambalo ni kosa kisheria. Baadhi ya ramani hizi hazitoi tafsiri sahihi ya mipaka na hasa mipaka ya nchi yetu na nchi jirani. **Natoa rai kwa wote wanaojihusisha na shughuli hizo waache mara moja vinginevyo Wizara haitasita kuwachukulia hatua za kisheria**

ikiwa ni pamoja na kuwafikisha mahakamani.

Ramani ya mipaka halisi ya Tanzania ni kama inavyoonekana nyuma ya kitabu hiki.

Mipaka ya Ndani ya Nchi

48) **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2016/17 Wizara iliahidi kukamilisha uhakiki wa sehemu ya mpaka wa Hifadhi ya Ngorongoro wenye urefu wa kilomita **83.6** kwa kushirikiana na wadau wengine. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa kazi hii imekamilika. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais- TAMISEMI; Wizara ya Maliasili na Utalii; Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi na Hifadhi ya Mamlaka ya Ngorongoro na Hifadhi ya Serengeti, inaendelea kuainisha mipaka ya ushoroba wenye ukubwa wa kilomita za mraba **2,500** katika pori tengefu la Loliondo wilayani Ngorongoro.

Mipaka ya Kimataifa

49) **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2016/17, Wizara iliahidi kuanza kazi ya upigaji picha za anga katika mpaka wa Tanzania na Kenya wenye urefu wa kilomita **756**. Upigaji picha za anga kwenye mpaka huo umekamilika. Vilevile uhakiki wa ubora wa picha hizo umefanyika na

kukamilika. Katika mwaka wa fedha 2017/18 Wizara itaendelea na uimarishaji wa mpaka wa Tanzania na Kenya ikiwa ni pamoja na utengenezaji wa ramani za msingi pamoja na kupima kipande cha mpaka kuanzia Ziwa Victoria hadi Ziwa Natron chenye urefu wa kilomita 240. Aidha, majadiliano kati ya Tanzania na Zambia na Tanzania na Uganda kwa ajili ya uimarishaji wa mipaka yanaendelea.

Upimaji wa Viwanja na Mashamba

50) ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2016/17, Serikali iliahidi kuidhinisha ramani za upimaji zenye viwanja **200,000** na mashamba **400**. Hadi kufikia 15 Mei, 2017, ramani za upimaji zenye jumla ya viwanja **118,502** na mashamba **374** ziliidhinishwa. Katika mwaka wa fedha 2017/18 Wizara itaidhinisha ramani za upimaji zenye jumla ya viwanja **200,000** na mashamba **400**.

51) ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2016/17 Wizara iliahidi kusimika na kupima alama za msingi za upimaji (*control points*) **200**. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2017, Wizara ilikuwa imesimika alama za msingi **154**

katika Halmashauri za Manispaa ya Morogoro (44), Dodoma (60), Manispaa ya Ubungo (30) na Halmashauri ya wilaya ya Buchosa (20). Alama hizi ni nyongeza katika alama za msingi zilizosimikwa katika mfumo mpya kusaidia shughuli za upimaji hapa nchini. Katika mwaka 2017/18 Wizara itasimika alama za msingi 200 kwa ajili ya kusaidia upimaji katika halmashauri mbalimbali nchini.

52) **Mheshimiwa Spika**, kumekuwa na changamoto ya kuandaa ramani hati (*deed plan*) ambazo ni muhimu katika kuandaa hatimiliki. Katika mwaka wa fedha 2016/17, Wizara yangu imeboresha utaratibu wa kuandaa ramani za hati. Kuanzia sasa ramani hizo zitaandaliwa kwenye ofisi za kanda za ardhi ili kurahisisha na kuharakisha uandaaji wa hatimiliki. Aidha, Wizara itatoa mafunzo kwa warasimu ramani (*cartographers*) wa halmashauri ili ramani hati ziandaliwe katika ngazi ya halmashauri kwa lengo la kupunguza urasimu, muda na gharama za kuandaa hatimiliki.

Upimaji wa Ardhi Chini ya Maji

- 53) **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/17, Wizara yangu iliahidi kuanza kazi ya upimaji ardhi chini ya maji katika bandari ya Tanga. Wizara kwa kushirikiana na Jeshi la Wanamaji la India, Mamlaka ya Bandari na Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) Kikosi cha Wanamaji imekamilisha upimaji chini ya maji katika bandari ya Tanga.

Kujenga uwezo wa kupima ardhi nchini

- 54) **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2017/18 Wizara yangu kupitia mradi wa *Private Sector Competitiveness Project (PSCP)* itanunua vifaa vya kisasa vyenye ufanisi mkubwa katika upimaji wa ardhi. Vifaa hivyo vitapelekwa katika ofisi za kanda ili kurahisisha upimaji na pia itatoa mafunzo kwa wataalam wa upimaji watakaotumia vifaa hivyo. Vifaa hivyo vimegawanyika katika makundi matatu, kundi la kwanza linajumuisha vifaa vinavyopima mfululizo ili kupata takwimu za hali ya nchi (*Continuous Operating Reference Stations CORS*), kundi la pili ni vifaa vya upimaji wa ardhi vinavyotumia simu na inteneti (RTK-GPS), na kundi la tatu ni vifaa vya kuchora ramani (*digital photogrammetric workstations*).

Utayarishaji wa Ramani Picha

55) **Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu imekamilisha uandaaji wa Ramani Picha (*orthorectified image*) za Jiji la Dar es Salaam. Ramani picha hizo zitatumika katika ujenzi wa Mfumo Unganishi wa Kuhifadhi Kumbukumbu za Ardhi (ILMIS). Katika mwaka wa fedha 2017/18 Wizara itatumia ramani picha hizo katika kuhuisha ramani za msingi, kubuni na kuandaa mipango mbalimbali ya maendeleo katika Jiji la Dar es Salaam.

Halmashauri ya Taifa ya Wapima

56) **Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu kupitia Halmashauri ya Taifa ya Wapima na Wathamini imeendelea kusimamia maadili ya taaluma ya wapima ardhi na wathamini nchini. Katika siku za karibuni kumekuwa na wimbi kubwa la watu wasiosajiliwa kujihusisha na shughuli za upimaji ardhi na uthamini na kuwa chanzo cha migogoroya ardhi nchini. Ili kukabiliana na tatizo hili, Wizara yangu imechukua hatua kwa kufanya uhakiki wa makampuni ya upimaji na wapima ardhi wa makampuni hayo. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2017 Halmashauri ilikuwa imesajili makampuni **67** ya upimaji ardhi na **58** ya uthamini nchini.

Natoa wito kwa umma kutumia makampuni na wataalam waliosajiliwa.

HUDUMA ZA UPANGAJI MIJI NA VIJJI

57) **Mheshimiwa Spika**, kuratibu na kusimamia upangaji na uendelezaji wa miji na vijiji ni mojawapo ya majukumu ya Wizara yangu. Utekelezaji wa jukumu hili unalenga kuwa na makazi yaliyopangwa, kuhifadhi mazingira na uhakika wa uwekezaji katika ardhi.

Mipango Kabambe ya Uendelezaji Miji (*Master Plans*)

58) **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2016/17, Wizara iliahidi kushirikiana na Halmashauri za Jiji la Mwanza na Arusha kukamilisha mipango kabambe ya majiji hayo. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa mipango kabambe hiyo imekamilika. Aidha, Wizara iliahidi kushirikiana na Jiji la Mbeya, Manispaa za Moshi, Bukoba, Mpanda na Lindi na Halmashauri ya Mji wa Babati kuandaa mipango kabambe ya miji hiyo. Utayarishaji wa mipango kabambe ya miji hiyo ipo katika hatua mbalimbali za uandaaji. Vilevile, Wizara iliahidi kuidhinisha mipango kabambe ya majiji ya Dar es Salaam, Mwanza, Arusha na Tanga; Manispaa za Iringa,

Musoma, Tabora, Mtwara, Sumbawanga, Songea, Singida pamoja na Miji ya Bariadi, Kibaha na Korogwe. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2017, mipango kabambe ya Manispaa za Musoma na Mtwara imekamilika na kuzinduliwa rasmi. Mipango kabambe iliyobaki ipo katika hatua za kukamilishwa na kuidhinishwa (**Jedwali Na.10**).

- 59) ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2017/18, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri husika itakamilisha mipango kabambe ya majiji ya Dar es Salaam na Tanga; Manispaa ya Singida pamoja na miji ya Ifakara, Mahenge, Malinyi, Bariadi, Kibaha na Korogwe. Aidha, Wizara itaendelea kupokea na kuidhinisha mipango kabambe kadri itakavyopokelewa kutoka Mamlaka za Upangaji. **Naendelea kusisitiza kuwa Halmashauri zote nchini zitenge fedha ya kuwezesha kuandaa mipango kabambe ili kuwa na miji iliyopangwa. Aidha, Halmashauri zihakikishe kuwa uendelezaji miji unazingatia mipango kabambe husika kwa lengo la kuepuka ukuaji holela wa miji.**

Usanifu na Uendelezaji wa Miji

- 60) ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha wa 2016/17, Wizara iliahidi kupokea, kukagua

na kuidhinisha jumla ya michoro ya mipangomiji **2,000** kutoka Mamlaka za Upangaji. Jumla ya michoro ya Mipangomiji **1,428** ilipokelewa kutoka halmashauri mbalimbali nchini. Kati ya hiyo, michoro **1,029** yenye jumla ya viwanja **401,607** iliidhinishwa na kuhifadhiwa. Michoro **399** ilirudishwa katika Halmashauri husika ili ifanyiwe marekebisho. Katika mwaka wa fedha 2017/18, Wizara inatarajia kupokea, kukagua na kuidhinisha jumla ya michoro ya mipangomiji **2,000** kutoka mamlaka za upangaji.

- 61) ***Mheshimiwa Spika***, Wizara iliahidi kukamilisha Mpango wa Uendelezaji upya eneo la Kurasini katika Jiji la Dar es Salaam. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Mpango huo umekamilika na eneo linatumika kwa shughuli zinazohusiana na bandari. Kadhalika kwa kushirikiana na mamlaka za upangaji iliahidi kutangaza vituo vya huduma pembezoni mwa miji katika miji ya Mwanza, Arusha, Musoma, Mtwara, Iringa, Shinyanga, Singida, Songea, Tanga, na Tabora. Hadi tarehe 15 Mei, 2017 jumla ya vituo **30** vilikuwa vimetambuliwa kwa mchanganuo ufuatao: Mwanza (**2**), Arusha (**3**), Musoma (**3**), Mtwara (**4**), Iringa (**3**), Shinyanga (**4**), Tabora (**6**) na Kibaha (**5**).

Usimamizi na Udhhibiti wa Uendelezaji Miji

62) **Mheshimiwa Spika**, mabadiliko ya matumizi ya ardhi, mgawanyo wa mashamba na viwanja unalenga kutumia ardhi na miundombinu kwa ufanisi, kuruhusu uwekezaji mpya na kuongeza thamani ya ardhi. Katika mwaka wa fedha 2016/17 Wizara kwa kushirikiana na halmashauri nchini iliendelea kusimamia na kudhibiti uendelezaji wa miji na kupunguza matumizi kinzani. Katika mwaka huu wa fedha, Wizara yangu ilipokea jumla ya maombi **334** ya mabadiliko ya matumizi ya ardhi, na mgawanyo/muunganiko wa viwanja na mashamba kutoka Halmashauri mbalimbali nchini. Maombi **187** yaliidhinishwa, maombi **49** yalikataliwa kutokana na kutokidhi vigezo, maombi **29** yalirudishwa katika halmashauri husika kwa ajili ya kufanyiwa marekebisho mbalimbali na maombi **69** yapo kwenye hatua za uhakiki.

63) **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara yangu itaanza kuidhinisha maombi ya mabadiliko ya matumizi ya ardhi, mgawanyo wa viwanja na mashamba katika ofisi za kanda ili kusogeza huduma karibu na wananchi. Vilevile, Wizara yangu inatarajia

kuandaa mwongozo wa kuziwezesha mamlaka za upangaji nchini kusimamia na kudhibiti uendelezaji wa miji katika ngazi za Halmashauri, Mitaa na Vijiji ili kuwa na miji endelevu na kupunguza migogoro ya ardhi.

Urasimishaji wa Makazi Holela Mijini

64) **Mheshimiwa Spika**, kwa kushirikiana na Mamlaka za Upangaji, Serikali inatekeleza kwa awamu Programu ya Taifa ya Kurasimisha Makazi na Kuzuia Ujenzi Holela Mijini (2013 – 2023). Katika mwaka wa fedha 2016/17, Wizara iliahidi kuendelea na urasimishaji makazi **6,000** katika Kata za Kimara na Saranga katika Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo. Aidha, Wizara iliahidi kushirikiana na Halmashauri za Manispaa za Sumbawanga, Singida, Musoma, Kigoma Ujiji, Lindi na Tabora kurasimisha makazi **3,000** kwa kila Halmashauri. Hadi tarehe 15 Mei, 2017 jumla ya makazi **4,333** kati ya **6,000** yalirasimishwa na uchongaji wa barabara zenye urefu wa kilomita **9.1** ulifanyika katika kata ya Kimara katika Manispaa ya Ubungo.

65) **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2016/17 Wizara yangu iliahidi kuendelea kuratibu utekelezaji wa Programu ya Taifa ya Kurasimisha

Makazi na Kuzuia Ujenzi Holela Mijini (2013-2023). Ili kufikia dhamira ya Programu hii, Serikali imetoa elimu na kugawa miongozo ya urasimishaji kwa wataalam **97** wa sekta ya ardhi katika Halmashauri **12** za Musoma, Mwanza, Kigoma Ujiji, Tabora, Lindi, Nzega, Singida, Iringa, Mbeya, Tunduma, Sumbawanga na Mtwara. Aidha, michoro ya urasimishaji kutoka halmashauri mbalimbali yenye jumla ya vipande vya ardhi **53,764** iliidhinishwa (**Jedwali Na.11**). Pia utafiti wa awali uliofanyika katika halmashauri sita (**6**) za Musoma, Kigoma Ujiji, Singida, Tabora, Sumbawanga na Lindi umeonesha maeneo yenye jumla ya makazi **50,200** yanaweza kurasimishwa chini ya mradi wa *Private Sector Competitiveness Project* (PSCP).

Upangaji wa Makazi ya Vijiji

66) **Mheshimiwa Spika**, upangaji wa makazi vijijini unalenga kudhibiti ukuaji holela wa maeneo hayo ambayo yanatarajiwa kuwa miji ya baadaye. Katika mwaka wa fedha wa 2017/18, Wizara itaendelea kuzijengea uwezo Halmashauri za wilaya tano katika uandaaji wa mipango kina ya makazi na vituo vya biashara. Halmashauri hizo ni Kilombero, Ulanga, Malinyi, Mbeya na Iringa.

Utengaji wa Maeneo ya Ujenzi wa Viwanda

67) **Mheshimiwa Spika**, katika kushiriki kutimiza azma ya Serikali ya kujenga uchumi wa viwanda, jumla ya ekari **83,080** zimeainishwa katika maeneo ya mipango kabambe katika halmashauri **14** nchini kwa ajili ya ujenzi wa viwanda (**Jedwali Na.12**). Hili ni ongezeko la ekari **19,050** ikilinganishwa na maeneo yaliyoainishwa katika mwaka wa fedha 2015/16. Katika mwaka wa fedha 2017/18 Wizara itaendelea kuhimiza halmashauri zinazoandaa mipango kabambe kuendelea kutenga maeneo zaidi kwa ajili ya viwanda.

Wakala wa Uendelezaji Mji Mpya wa Kigamboni (KDA)

68) **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha wa 2016/17 Wizara kupitia KDA iliahidi kuendelea kuandaa mipangokina ya matumizi ya ardhi katika eneo lote la mpango, kuanisha na kupima maeneo ya miundombinu na huduma za umma, kufanya uthamini na kulipa fidia, kukamilisha mpango mkakati wa KDA wa miaka mitano (2016/17-2020/21). Hadi tarehe 15 Mei, 2017, mipangokina **28** yenye viwanja **4,500** vya matumizi mbalimbali ya ardhi imeandaliwa na kuidhinishwa tayari kwa upimaji wa viwanja

husika. Pia barabara kuu zenye urefu wa kilomita **59.8** zimepimwa na kusimikwa mawe ya mpaka. Vilevile, hatimiliki **256** zimetolewa katika eneo la Mji mpya wa Kigamboni na vibali vya ujenzi **15** zimetolewa kwa waendelezaji wa ardhi. Rasimu ya Mpango mkakati wa Wakala wa miaka mitano iliandaliwa (2017-2022).

- 69) ***Mheshimiwa Spika***, pamoja na juhudi zinazofanywa na KDA katika kuendeleza mji wa Kigamboni, kumekuwa na maoni ya baadhi ya wadau kwamba majukumu ya KDA yatekelezwe na Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni. Hivyo, Serikali inayafanyia kazi maoni haya pamoja na mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii ili kuona namna bora zaidi ya kusimamia uendelezaji wa Mji Mpya wa Kigamboni.

Bodi ya Usajili wa Wataalam wa Mipangomiji

- 70) ***Mheshimiwa Spika***, jukumu kubwa la Bodi ya Wataalam wa Mipangomiji ni kusajili wataalam na makampuni na kudhibiti utendaji wa wataalam na makampuni katika fani hii. Vilevile, Bodi hii ina jukumu la kusimamia weledi na kutoa adhabu stahiki kwa wataalam na makampuni

yanayokiuka taratibu na sheria zinazosimamia upangaji miji na vijiji. Shughuli hii inafanywa kulingana na Sheria ya Usajili wa Wataalam wa Mipangomiji Na. 7 ya Mwaka 2007. Katika mwaka wa fedha 2016/17, Bodi ilisajili jumla ya wataalam **31** na kufanya idadi ya wataalam waliosajiliwa kufikia **306**. Kadhalika katika kipindi hicho, Bodi ilisajili makampuni **8** na kufikisha jumla ya makampuni **40** ya mipangomiji na vijiji. Aidha, Bodi ilifuta usajili wa wataalam **16** na kutoa onyo kwa mtaalam mmoja (**1**). Katika mwaka wa fedha 2017/18 Bodi itaendelea kusajili wataalam na makampuni yatakayokidhi vigezo na kuchukua hatua stahiki kwa wataalam wasio waadilifu na makampuni yasiyofuata taratibu kwa mujibu wa sheria.

FUNGU 03: TUME YA TAIFA YA MIPANGO YA MATUMIZI YA ARDHI

71) **Mheshimiwa Spika**, Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi inatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Na.6 ya mwaka 2007. Sheria hiyo inaipa Tume mamlaka ya kupanga matumizi ya ardhi yote nchini kwa azma ya kutumia vizuri rasilimali zote za ardhi ili kuondoa umaskini na kuleta maendeleo endelevu.

Mpango wa Taifa wa Matumizi ya Ardhi (2013 – 2033)

72) **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2016/17, Wizara yangu kupitia Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi iliendelea kutekeleza Mpango wa Taifa wa Matumizi ya Ardhi kwa kufanya uhamasishaji wa Mpango na kutoa mafunzo kwa watendaji (Timu za Usimamizi wa Ardhi za Wilaya) wa Halmashauri za Wilaya **24**. Mafunzo hayo yalihusu mbinu shirikishi za uandaaji, utekelezaji na usimamizi wa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji. Halmashauri hizo ni Mbeya, Ulanga, Kilombero, Kisarawe, Kilwa, Chamwino, Urambo, Geita, Bahi, Kongwa, Kilolo, Mufindi, Madaba, Njombe, Ludewa, Makete,

Mbinga, Nyasa, Mvomero, Tanganyika, Serengeti, Liwale, Newala na Tarime.

73) **Mheshimiwa Spika**, Tume kwa kushirikiana na Taasisi ya *Ujamaa Community Resource Team*, Jumuiiko la Maliasili Tanzania, HakiArdhi, Umoja wa Waandishi wa Habari za Ardhi na Mazingira na mashirika ya kimataifa ya *Care International* na *Oxfam*, iliendelea kutoa elimu kwa umma juu ya malengo na umuhimu wa Mpango wa Taifa wa Matumizi ya Ardhi, utekelezaji wake na mchango wake katika kutatua migogoro ya matumizi ya ardhi nchini. Elimu hii ilitolewa kupitia vyombo vya habari ambapo jumla ya vipindi maalum **8** vilirushwa hewani kupitia televisheni na radio.

74) **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2017/18, Tume itafanya mapitio ya Programu za Mpango wa Taifa wa Matumizi ya Ardhi 2013-2033. Lengo likiwa ni kuhuisha na kujumuisha masuala ya maendeleo ya viwanda nchini ili kuendana na azma ya Serikali ya kujenga uchumi wa viwanda.

Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Wilaya na Vijiji

75) **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2016/17, Wizara yangu iliahidi kuandaa mipango

ya matumizi ya ardhi ya wilaya **5** na vijiji **1,500** kwa kushirikiana na wadau mbalimbali. Hadi kufikia tarehe 15 Mei 2017, Tume imewezesha kuandaliwa kwa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji **91** katika Wilaya **23**. Kazi hii imefanyika kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wakiwemo USAID, DFID, SIDA, DANIDA, Mradi wa Misitu ya Asili (PFP), Halmashauri za Wilaya ya Geita, Wilaya ya Kilwa, Chuo cha Mipango Dodoma, Taasisi za *LECIDE*, *PELUM Tanzania*, *African Wildlife Foundation (AWF)* na *Frankfurt Zoological Society*.

- 76) ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2017/18, Tume itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali ili kuongeza kasi ya kupanga matumizi ya ardhi nchini na kufikia lengo la Vijiji **1,500** na Wilaya **5** kwa mwaka. Ili kuweza kufikia lengo hili na kutatua changamoto mbalimbali zinazokabili upangaji, utekelezaji na usimamizi wa matumizi ya ardhi nchini, Tume kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeandaa mkakati na mpango kazi ambao utatekelezwa na wadau wote ili kufikia lengo hilo. **Natoa rai kwa sekta binafsi na wadau mbalimbali wa maendeleo washirikiane na Tume ili kuongeza kasi ya upangaji wa matumizi ya ardhi ya vijiji na wilaya ili kuondoa migogoro ya ardhi.**

MAENDELEO YA SEKTA YA NYUMBA

77) **Mheshimiwa Spika**, sekta ya nyumba hutoa mchango mkubwa katika kukuza uchumi kwa kuwapatia wananchi siyo tu makazi bali pia inaongeza fursa za ajira na kupunguza umaskini, kuchangia mapato ya Serikali na kuongeza pato la Taifa. Ili kuwezesha sekta hii kufikia malengo hayo, Serikali imeendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji kwa kurahisisha upatikanaji wa mitaji kwa ajili ya upatikanaji wa mikopo ya nyumba. Pia Wizara yangu imekuwa ikihimiza Shirika la Nyumba la Taifa, taasisi za Serikali, sekta binafsi na wadau wengine kuongeza kasi ya uwekezaji katika sekta ya nyumba ili kupunguza uhaba mkubwa wa nyumba uliopo nchini.

78) **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2016/17, Wizara imeendelea kufuatilia maendeleo ya sekta ya nyumba nchini. Mwamko wa taasisi za fedha wa kutoa mikopo kwa ajili ya ujenzi wa nyumba unaongezeka mwaka hadi mwaka. Hadi sasa jumla ya benki **28** zimeshatoa mikopo ya nyumba yenye thamani ya zaidi ya shilingi bilioni **416**. Serikali imekuwa ikitoa fedha kupitia taasisi ya *Tanzania Mortgage Refinancing Company* (TMRC) ili kuziwezesha benki kutoa

mikopo ya nyumba kwa wananchi. Hadi sasa zaidi ya wananchi **1,210** wamefaidika na mikopo yenye thamani ya zaidi ya shilingi bilioni **126**. Vilevile, Serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania inatoa mikopo ya nyumba kwa taasisi ndogondogo za fedha (*microfinance*) ili zitoe mikopo ya uendelezaji wa nyumba yenye masharti nafuu kwa wananchi wa kipato cha chini. Hadi sasa wananchi wapatao **574** wamefaidika na mikopo hiyo ambayo jumla yake ni zaidi ya shilingi bilioni tisa (**9**).

- 79) **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2016/17, Wizara yangu imeendelea kukusanya taarifa za waendelezaji milki na kuingizwa katika kanzidata. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2017, kanzidata hiyo ina jumla ya waendelezaji milki **127** na nyumba **17,813**. Katika mwaka wa fedha 2017/18 Wizara yangu kupitia mradi wa *Housing Finance Project* unaosimamiwa na Benki Kuu ya Tanzania itaboresha kanzidata ya nyumba nchini kwa kujumuisha taarifa za soko la nyumba kama vile bei za nyumba na kodi ya pango la nyumba. Aidha, Wizara yangu itaratibu uandaaji wa mwongozo na viwango vya ujenzi wa nyumba za gharama nafuu (*Guidelines and Standards for Affordable Housing*) lengo ni kuwa na viwango vya ujenzi wa nyumba za watu wa kipato cha chini nchini.

Mfuko wa Mikopo ya Nyumba kwa Watumishi wa Serikali

80) **Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu inasimamia Mfuko wa Mikopo ya Nyumba kwa Watumishi wa Serikali ulioanzishwa kupitia Waraka wa Serikali Na. 8 wa mwaka 1992. Lengo la Mfuko huo ni kuwawezesha watumishi kupata mikopo ya kujenga, kukarabati ama kununua nyumba. Katika mwaka wa fedha 2016/17 watumishi wa Serikali **80** wamepatiwa mikopo ya jumla ya shilingi milioni **743**. Vilevile, katika kipindi hicho Wizara imekusanya marejesho ya jumla ya shilingi milioni **500.6**. Katika mwaka 2017/18 Wizara yangu itaendelea kupokea na kushughulikia maombi mapya na kukusanya marejesho kulingana na taratibu za mfuko.

Ushirikiano na Taasisi za Makazi za Kimataifa

81) **Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu inaratibu ushirikiano wa kimataifa katika masuala ya makazi. Katika mwaka wa fedha 2016/17 Wizara kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo ya makazi nchini iliadhimisha siku ya makazi duniani mnamo tarehe 3 Oktoba, 2016. Katika maadhimisho hayo, Wizara ilitumia fursa hiyo kuwaelimisha wananchi juu ya umuhimu wa kutekeleza lengo la 11 la Mpango wa Umoja

wa Mataifa wa Maendeleo Endelevu. Lengo hili linahusu kuwa na Miji na Makazi Salama, Imara na Endelevu. Aidha, Wizara ilishiriki katika Mkutano Mkuu wa III wa makazi ulioandaliwa na Shirika la Makazi la Umoja wa Mataifa (UN-Habitat) mjini Quito, Ecuador, Oktoba, 2016. Ajenda Mpya ya Makazi Duniani (*New Urban Agenda*) ilipitishwa kwa ajili ya kutekelezwa na nchi wanachama kama dira ya uendelezaji makazi kwa kipindi cha miaka 20 ijayo (2016-2036).

Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba na Vifaa vya Ujenzi (NHBRA)

82) **Mheshimiwa Spika**, Wakala umeendelea kufanya utafiti wa vigae vya kuchoma kwa ajili ya kuezekea vinavyotokana na udongo wa mfinyanzi, matofali ya kuchoma yanayofungamana, uboreshaji wa nyumba za udongo na matofali ya udongo, ujenzi wa sakafu (*suspended floor*) na utafiti wa kiasi cha nishati kinachotumika katika ujenzi wa nyumba.

83) **Mheshimiwa Spika**, utafiti mwingine uliofanywa ulihusu mashine ya kufyatua matofali mawili kwa nguvu za kunyonga baisikeli (*Tricycle Bricks Making Machine*) na mashine ya kufyatua matofali mawili inayoendeshwa kwa

kutumia dizeli (*Hydraulic brick making machine*), kwa kushirikiana na taasisi ya NYUMBU. Utafiti mwingine ni kutengeneza fremu za milango na madirisha kwa kutumia zege, matofali ya saruji yanayofungamana yenye kuhitaji kiasi kidogo cha plasta na matofali ya kufungamana ya kujengea matenki ya mviringo ya kuhifadhia maji.

- 84) ***Mheshimiwa Spika***, ili kusambaza matokeo ya tafiti hizo, hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2017 jumla ya mashine **133** za kufyatulia matofali ya kufungamana na vigae **53,389** vilitengenezwa na kuuzwa kwa wateja mbalimbali wa Wakala. Aidha, Wakala kwa kushirikiana na kampuni ya *Green Resources Ltd* uliendesha mafunzo ya vitendo kuhusu ujenzi wa nyumba bora za gharama nafuu kwa wananchi **173** kutoka wilaya mbalimbali. Vilevile, Wakala ulishiriki katika maonesho mbalimbali ili kusambaza matokeo ya tafiti yaweze kuwafikia wananchi walio wengi. Katika mwaka wa fedha 2017/18, Wakala utaendelea kufanya tafiti mbalimbali na kusambaza matokeo ya tafiti hizo kwa wananchi.

SHIRIKA LA NYUMBA LA TAIFA

Miradi ya Ujenzi wa Nyumba

85) ***Mheshimiwa Spika***, Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) liliendelea kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Na. 2 ya mwaka 1990 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2005. Shirika limeendelea kutekeleza majukumu yake ili kumudu ushindani wa kibiashara katika ujenzi wa nyumba za kuuza na kupangisha ikijumuisha nyumba za gharama nafuu. Katika mwaka wa fedha 2016/17, Shirika liliahidi kuendelea kukamilisha miradi iliyopo katika mikoa mbalimbali pamoja na kuendelea kujenga nyumba za gharama nafuu.

86) ***Mheshimiwa Spika***, katika Hotuba ya bajeti ya Wizara ya mwaka wa fedha 2016/17 suala la ujenzi wa nyumba za gharama nafuu liligusa hisia za Waheshimiwa Wabunge wengi na waliitaka Serikali kuangalia upya suala hili. Wizara yangu imeendelea kulihimiza Shirika la Nyumba kuweka kipaumbele katika ujenzi wa nyumba za gharama nafuu na kuzihamasisha Halmashauri kulipatia Shirika ardhi nafuu ya kujenga nyumba hizo. Aidha, taasisi na halmashauri zimeshaelekezwa

na Serikali kuweka miundombinu ya umeme, maji na barabara katika maeneo yanayojengwa nyumba na NHC ili kupunguza gharama za ujenzi wa nyumba hizo.

- 87) **Mheshimiwa Spika**, hadi sasa Shirika limekamilisha ujenzi wa miradi **29** kati ya miradi **54** iliyokuwa inatekelezwa. Miradi hiyo ni ya nyumba za gharama nafuu, gharama ya kati na juu, majengo ya biashara na majengo ya matumizi mchanganyiko na ina jumla ya nyumba **1,686**. Jumla ya miradi ya nyumba za gharama nafuu ni **14** na ina idadi ya nyumba **492**; miradi **10** ni ya nyumba za gharama ya kati na juu na ina jumla ya nyumba **881**; miradi **4** ni ya nyumba za biashara na ina nyumba **229** na jengo moja (1) ni la matumizi mchanganyiko na lina nyumba **84**. Aidha, jumla ya miradi **25** yenye jumla ya nyumba **4,126** inaendelea kujengwa. Kati ya hiyo, miradi **14** ni ya nyumba za gharama nafuu na ina jumla ya nyumba **1,002**; miradi **3** ni ya nyumba za gharama ya kati na juu na ina nyumba **760**; miradi **5** ni ya nyumba za biashara na ina nyumba **203**; na miradi **4** ni ya nyumba za matumizi mchanganyiko na ina nyumba **2,161**.

88) **Mheshimiwa Spika**, katika kuunga mkono uamuzi wa Serikali wa kuhamishia rasmi Makao Makuu Dodoma, Shirika limetoa kipaumbele katika ujenzi wa nyumba za makazi kwa ajili ya watumishi na wananchi wengine watakaohamia Dodoma. Katika mwaka wa fedha 2016/17 Shirika limeendelea kukamilisha awamu ya kwanza ya ujenzi wa nyumba **300** katika eneo la Iyumbu, Dodoma. Aidha, katika mwaka wa fedha 2017/18 Shirika litaendelea na awamu ya pili ya ujenzi wa nyumba katika eneo la Iyumbu na kukamilisha taratibu za kupata ardhi ya kujenga nyumba mjini Dodoma.

Mauzo na Makusanyo ya Kodi ya Pango la Nyumba

89) **Mheshimiwa Spika**, hadi tarehe 15 Mei, 2017 Shirika lilikuwa limekusanya jumla ya Shilingi bilioni **39** kutokana na mauzo ya nyumba. Aidha, katika mwaka wa fedha 2016/17 Shirika lilitarajia kukusanya kodi ya pango kiasi cha shilingi bilioni **86.59**. Hadi tarehe 15 Mei, 2017 makusanyo ya kodi ya pango yalifikia shilingi bilioni **88.28** ambayo ni sawa na asilimia **102** ya lengo la mwaka. Katika mwaka 2017/18 Shirika linatarajia kukusanya kodi ya pango kiasi cha shilingi bilioni **95.10 (Jedwali 13)**.

Uendelezaji wa Vitovu vya Miji

90) **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2016/17, Shirika liliendelea kutekeleza miradi ya Vitovu vya Miji (*Satellite Cities*) kama Mwendelezaji Mkuu katika maeneo ambayo Shirika linamiliki ardhi. Miradi hii ni pamoja na Kawe ambapo mpangokina upo katika hatua za mwisho za kuidhinishwa na ujenzi wa nyumba unaendelea; Safari City ulioko Arusha ambako ujenzi wa nyumba **10** za mfano na uuzaji wa viwanja unaendelea; ujenzi wa nyumba **300** katika eneo la Iyumbu Dodoma na Usa River ambapo mpangokina umepitishwa na mkandarasi wa kujenga nyumba za mfano amepatikana. Katika mwaka wa fedha 2017/18, Shirika litaendelea kupanga na kuendeleza maeneo ya vitovu vya Kunduchi Rifle Range, Songwe, Ruvu, Pembamnazi, Chato na Kibondo.

Ardhi kwa ajili ya Ujenzi wa Nyumba

91) **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2016/17, Shirika liliongeza akiba ya ardhi kiasi cha ekari **112.74**. Katika mwaka wa fedha 2017/18, Shirika kwa kushirikiana na halmashauri za miji na wilaya na wadau wengine katika kutekeleza agizo la Serikali litahakikisha kuwa ardhi yake inawekewa miundombinu ya

umeme, barabara na maji kabla ya kuanza kwa ujenzi. Hatua hii itachangia kwa kiasi kikubwa kupunguza gharama za nyumba hususan nyumba za wananchi wa kipato cha chini.

HUDUMA ZA KISHERIA NA SERA

Huduma za Kisheria

92) **Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu imeendelea kusimamia sekta ya ardhi kwa kuzingatia sheria zilizopo. Katika mwaka 2016/17, Wizara iliahidi kuandaa mapendekezo ya kutunga na kuhuisha sheria mbalimbali zinazohusu sekta ya ardhi. Kazi zilizofanyika katika kipindi hiki ni kutunga Sheria ya Uthamini na Usajili wa Wathamini Na. 7 ya mwaka 2016 ambayo ilianza kutumika rasmi tarehe 1 Januari, 2017 baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali Na. 1 la tarehe 6 Januari, 2017. Aidha, ili kusimamia na kuendeleza sekta ya milki, kuhuisha utaratibu wa utwaaji ardhi na kusimamia mawakala wa ardhi, Wizara yangu imeandaa rasimu za miswada ya Sheria ya Usimamizi wa Uendelezaji Milki, Sheria ya Utwaaji Ardhi na Fidia na Sheria ya Mawakala wa Ardhi.

93) **Mheshimiwa Spika**, vilevile, Wizara imeandaa rasimu ya Marekebisho ya Sheria ya Mipangomiji Na. 8 ya mwaka 2007 ili kusogeza huduma za mipangomiji katika ngazi ya Kanda. Kadhalika, imeandaa rasimu ya Kanuni za Sheria ya Uthamini na Usajili wa Wathamini na kutunga kanuni za Mitihani kwa Maafisa wa Mipangomiji za mwaka 2016 zilizotangazwa katika Gazeti la Serikali Na. 277 la tarehe 5 Agosti, 2016. Kanuni hizi zinatumiwa na Bodi ya Usajili wa Maafisa Mipangomiji wakati wa kusajili wataalam hao. Aidha, rasimu ya tafsiri ya Kiswahili ya Sheria ya Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi Na. 2 ya mwaka 2002 imeandaliwa. Katika mwaka wa fedha 2017/18, Wizara itakamilisha rasimu za miswada ya Sheria ya Usimamizi wa Uendelezaji Milki, Sheria ya Utwaaji Ardhi na Fidia, Sheria ya Mawakala wa Ardhi na Kanuni za Sheria ya Uthamini na Usajili wa Wathamini.

Mapitio ya Sera

- 94) **Mheshimiwa Spika**, Wizara imekamilisha mapitio ya Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995 na kuandaa Rasimu ya marekebisho ya Sera hiyo kwa kushirikiana na wataalam washauri kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu Ardhi na sekta binafsi. Kwa ujumla, madhumuni ya mapitio ya Sera hiyo ni kuweka misingi ya kukabiliana na changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995. Lengo la marekebisho hayo ni kuimarisha usalama wa milki, kuboresha mazingira ya uwekezaji katika sekta ya ardhi, kudhibiti migogoro ya matumizi ya ardhi pamoja na kuhakikisha kwamba kila kipande cha ardhi kinapangwa, kupimwa na kumilikishwa.
- 95) **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2016/17, Wizara iliahidi kufanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000 na kuandaa Sera ya Nyumba. Wizara kwa kutumia wataalam washauri kutoka Chuo Kikuu Ardhi inaendelea na mapitio ya Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000 ili kuihuisha na kutayarisha rasimu ya Sera ya Nyumba. **Natoa wito kwa wadau wote kujitokeza kutoa maoni ili tuweze kupata sera zitakazokidhi mahitaji ya sasa na baadaye.**

Elimu kwa Umma

96) **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2016/17 Wizara iliahidi kuendelea kuelimisha umma kuhusu sera, sheria, kanuni na taratibu zinazosimamia sekta ya ardhi. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa elimu kwa umma ilitolewa kupitia vyombo mbalimbali vya habari ikiwemo luninga (vipindi 23), redio (vipindi 28) pamoja na machapisho, vipeperushi na jarida la Wizara ambapo nakala **2,500** zilichapishwa na kusambazwa. Aidha, elimu ilitolewa kupitia tovuti ya Wizara, mitandao ya kijamii, matangazo, mahojiano, makala maalum magazetini saba (7), taarifa kwa umma, mikutano 17 na semina mbili (2). Katika mwaka wa fedha 2017/18 Wizara itaendelea kuelimisha umma kuhusu sera, sheria, kanuni na taratibu zinazosimamia sekta ya ardhi.

HUDUMA ZA UTAWALA NA RASILIMALI WATU

97) **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2016/17, Wizara yangu iliahidi kuendelea kuboresha utoaji wa huduma kwa kuweka mifumo bora zaidi ya utendaji kazi na mazingira bora ya ofisi kwa lengo la kuleta ufanisi katika kazi. Pia Wizara iliahidi kuwapatia mafunzo watumishi 150

wa kada mbalimbali. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2017 Wizara imeendelea kuboresha mazingira ya ofisi kwa kununua vitendea kazi na kukarabati majengo ya ofisi. Vilevile Wizara iliandaa ofisi za Makao Makuu yake Mjini Dodoma. Aidha, jumla ya watumishi **491** wamehudhuria mafunzo ya muda mfupi na mrefu ndani na nje ya nchi. Katika mwaka wa fedha 2017/18, Wizara inatarajia kuwapatia mafunzo watumishi **70** na kuajiri watumishi **291**. Pia Wizara itaendelea kupanua na kuboresha ofisi zake ili kuwezesha watumishi wengi zaidi kuhamia Dodoma.

98) **Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu imeendelea kuboresha mazingira ya utendaji kazi kupitia Kituo cha Huduma kwa Mteja (*Customer Service Centre*) kilichopo katika Kanda ya Dar es Salaam. Kituo kimeweza kuwahudumia jumla ya wananchi **88,400** ambao ni sawa na wastani wa wateja **2,210** kwa wiki na wateja **442** kwa siku ikilinganishwa na wastani wa wateja **420** kwa siku katika mwaka 2015/16 waliofika kupata huduma mbalimbali zitolewazo na kituo. Dhamira ya Wizara ni kuwa na vituo vya huduma kwa mteja kwa kila ofisi ya kanda.

99) **Mheshimiwa Spika**, ufanisi kazini unategemea watumishi wenye afya bora. Katika mwaka wa fedha 2016/17, Wizara yangu imeendelea kuwaelimisha na kuwasisitiza watumishi kupima afya zao ili kujikinga na janga la UKIMWI na magonjwa mengine. Aidha, Wizara imeendelea kuwawezesha watumishi na familia zao wanaoishi na Virusi vya UKIMWI ambapo watumishi **20** wamewezeshwa kupata dawa na lishe.

Vyuo vya Ardhi Tabora na Morogoro

100) **Mheshimiwa Spika**, Wizara inaendelea kuviimarisha vyuo vya Morogoro na Tabora kwa kuendelea na ujenzi wa maktaba katika Chuo cha Ardhi Tabora, kuweka mfumo wa kielektroniki wa usajili wa wanafunzi na kununua vifaa na mitambo ya kufundishia na kujifunzia kwa vitendo ili kuwawezesha wanachuo kupata ujuzi unaokidhi viwango katika taaluma zao. Idadi ya wahitimu katika vyuo vya ardhi vya Morogoro na Tabora iliongezeka kutoka **495** mwaka 2015/16 hadi **559** mwaka 2016/17 (**Jedwali Na. 14**). Katika mwaka wa fedha 2017/18, Wizara itaendelea na ujenzi wa maktaba katika Chuo cha Ardhi Tabora na ununuzi wa samani kwa ajili ya maktaba ya Chuo cha Ardhi Morogoro.

C: CHANGAMOTO NA MIKAKATI YA KUKABILIANA NAZO

101) **Mheshimiwa Spika**, licha ya juhudi zilizotekelezwa na Wizara katika mwaka wa fedha 2016/17, Wizara bado inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

- i) Uratibu wa sekta ya ardhi kwa kuwa inasimamiwa na mamlaka zaidi ya moja;
- ii) Uhaba wa wataalam na vitendea kazi vinavyohitajika ili kukidhi utoaji wa huduma katika sekta ya ardhi;
- iii) Kasi ya ongezeko la idadi ya watu na mifugo ikilinganishwa na upatikanaji wa ardhi iliyopangwa na kupimwa;
- iv) Ucheleweshaji wa ulipaji wa fidia stahiki kwa ardhi iliyotwaliwa kwa ajili ya matumizi ya maendeleo; na
- v) Uelewa mdogo wa wananchi kuhusu sera na sheria za ardhi.

102) **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2017/18, hotuba yangu imeainisha mikakati mbalimbali itakayotekelezwa ili kukabiliana na changamoto hizo. Katika kuimarisha usalama wa milki pamoja na kuongeza kasi ya kupima na kupanga ardhi, Wizara imekamilisha mapitio ya

Sera ya Taifa ya mwaka 1995 kwa kushirikiana na wadau mbalimbali nchini.

103) **Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla, madhumuni ya mapitio ya Sera hiyo ni pamoja na kuziba mianya au viashiria vya migogoro ya matumizi ya ardhi baina ya watumiaji nchini, kuongeza kasi ya upimaji, upangaji na umilikishaji wa kila kipande cha ardhi na kuwawezesha wananchi wasio na ardhi vijijini kumiliki ardhi kwa shughuli za kilimo na ufugaji na kujenga mazingira bora yanayovutia uwekezaji nchini. Aidha, katika kuimarisha na kuendeleza sekta ya milki, Wizara kwa kushirikiana na watalaam washauri kutoka Chuo Kikuu Ardhi inapitia Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000 kwa lengo la kuihuisha zaidi kwa kuzingatia mazingira ya sasa ya mahitaji ya jamii ya makazi na nyumba.

104) **Mheshimiwa Spika**, kuhusu uhaba wa wataalam na vitendea kazi, Wizara inaendelea kuishirikisha sekta binafsi katika utekelezaji wa majukumu yake. Hadi 15 Mei, 2017 jumla ya kampuni binafsi za kupanga **38** na kupima ardhi **67** zilikuwa zimesajiliwa. Aidha, Wizara imepeleka vitendea kazi muhimu kwenye kanda ili kuimarisha utoaji wa huduma za ardhi karibu na wananchi yakiwemo magari.

105) **Mheshimiwa Spika**, Wizara inatekeleza programu ya kupanga, kupima na kumilikisha ardhi. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na halmashauri itaendelea kuhakiki viwanja na mashamba ambayo hayajaendelezwa kwa muda mrefu, kufuta milki na kuyapangia matumizi mengine. Vilevile, ili kupunguza au kudhibiti migogoro inayosababishwa na ucheleweshaji wa ulipaji wa fidia stahiki na kwa wakati, Serikali imeunda Bodi ya Mfuko wa Fidia ya Ardhi kwa ajili ya kuratibu masuala yote ya fidia nchini yakayofanywa na wizara na taasisi za mbalimbali. Aidha, Serikali inaendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu sheria, kanuni, taratibu na miongozo inayotawala sekta ya ardhi.

D: SHUKRANI

106) **Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Wizara yangu, naomba kumalizia hotuba yangu kwa kuwashukuru kwa dhati wadau wote wa sekta ya ardhi ikiwa ni pamoja na Serikali za Vijiji, Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Majiji. Vilevile napenda kuishukuru Benki ya Dunia na nchi wahisani zikiwemo Uingereza, Denmark, Sweden, Japan, China, India, Korea ya Kusini na Marekani. Wizara yangu inatambua na kuthamini michango inayotolewa na wadau wote wa sekta ya ardhi katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

107) **Mheshimiwa Spika**, kwa mara nyingine napenda kumshukuru Naibu Waziri wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mheshimiwa Dkt. Angelina Sylvester Lubala Mabula (Mb), kwa kunisaidia katika kutekeleza majukumu yangu. Pia napenda kumshukuru Katibu Mkuu Dkt. Yamungu Kayandabila na Naibu Katibu Mkuu Dkt. Moses Kusiluka kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa. Nawashukuru Wakuu wa Idara na Vitengo, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara pamoja na watumishi wote wa sekta ya ardhi katika ngazi zote kwa kunisaidia kutimiza majukumu yangu.

E: HITIMISHO

108) **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2017/18, Wizara itaendelea kushirikiana na Halmashauri zote kutayarisha mipango ya kuendeleza miji na vijiji, kusimamia upangaji, upimaji, urasimishaji, umilikishaji na usajili wa hati ili kuwezesha kuwepo kwa usalama wa milki. **Natoa rai kwa mamlaka na asasi mbalimbali pamoja na wadau wote wa sekta ya ardhi kutoa ushirikiano ili kuhakikisha kuwa ardhi inaziwezesha sekta zote kufikia malengo ya kumletea Mtanzania maendeleo na kuondokana na umaskini.**

F: MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2017/18

Makadirio ya Mapato

109) **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2017/18, Wizara inatarajia kukusanya jumla ya **Shilingi 112,050,000,000/=** kutokana na kodi, tozo na ada mbalimbali zinazotokana na shughuli za sekta ya ardhi kwa kutekeleza mikakati ambayo imeainishwa katika hotuba.

Makadirio ya Matumizi

110) **Mheshimiwa Spika**, ili Wizara yangu iweze kutekeleza majukumu niliyoyaeleza katika hotuba hii kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2017/18, sasa naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lijadili na kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Fungu **48**: Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Fungu **03**: Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi kama ifuatavyo:-

**Fungu 48: Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo
ya Makazi**

AINA	MAPATO/MATUMIZI	SHILINGI
A	Mapato ya Serikali	112,050,000,000
B	Matumizi ya Kawaida	
	Matumizi ya Mishahara	18,484,916,852
	Matumizi Mengineyo	24,770,166,074
	Jumla Ndogo	43,255,082,926
C	Matumizi ya Maendeleo	
	Fedha za Ndani	16,400,000,000
	Fedha za Nje	9,000,000,000
	Jumla Ndogo	25,400,000,000
	JUMLA KUU (B+C)	68,655,082,926

Jumla ya matumizi ya kawaida na maendeleo
Shilingi 68,655,082,926

**Fungu 03: Tume ya Taifa ya Mipango ya
Matumizi ya Ardhi**

AINA	MATUMIZI	SHILINGI
A	Matumizi ya Mishahara	1,135,550,000
B	Matumizi Mengineyo	979,821,822
	Jumla	2,115,371,822

Jumla ya matumizi ya kawaida ni **Shilingi 2,115,371,822/=**.

111) **Mheshimiwa Spika**, jumla kuu ya fedha zote zinazoombwa kwa Wizara (Fungu **48** na Fungu **03**) ni Shilingi **70,770,454,748/=**.

112) **Mheshimiwa Spika**, pamoja na hotuba hii yapo majedwali ambayo yanafafanua kwa kina utekelezaji wa majukumu, Randama na pia nimeambatisha vitabu viwili (2) vya taarifa za utekelezaji wa majukumu ambavyo ni sehemu ya hotuba yangu. Naomba taarifa hizo zichukuliwe kuwa ni vielelezo vya hoja hii. Hotuba hii pia inapatikana kwenye tovuti ya Wizara kwa anuani ya www.ardhi.go.tz.

113) **Mheshimiwa Spika**, mwisho natoa shukrani zangu za dhati kwako binafsi na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza.

114) **Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

MCHANGANUO WA MAPATO KWA MWAKA 2016/17

SEGMENT 4 (GFS CODE)	Ufafanuzi wa Vifungu	Makusanyo Halisi 2015/16	Malengo 2016/17	Makusanyo Halisi Hadi 15 Mei 2017	Makusanyo ikilingan- ishwa na lengo (%)
Idara ya Utawala na Rasilmali Watu					
140315	Receipts from Training and Examination Fee	590,173,500	720,000,000	759,993,411.35	105.6
140368	Miscellaneous Receipts	0	1,000	0	0.00
140370	Recovery of Public Money	0	1,000	0	0.00
Jumla ya Kifungu		590,173,500	720,002,000	759,993,411.35	105.6
Idara ya Utawala wa Ardhi					
140106	Rental Receipts – Lands	66,676,805,656.57	101,962,740,400	71,189,819,131.43	69.8
140330	Fee, Customary Tribunal and Land Tribunal	242,708,000	800,000,000	826,680,555	103.3
140329	Land Registration Fees	6,228,366,577.29	5,250,000,000	5,554,104,055.32	105.8
140256	Valuation Charges	958,810,606	3,000,000,000	2,175,841,421.96	72.5
140368	Miscellaneous Receipts	0	1,000	0	0
			1,000		

	Jumla ya Kifungu	74,106,690,839.48	111,012,741,40074.1 06,690,839.48	79,746,445,163.71	71.8
Idara ya Upimaji na Ramani					
140202	<i>Printing and Publications</i>	17,422,160	40,000,000	12,110,000	30.3
140257	<i>Reproduction Services</i>	0	1,000 1,000	0	0
140331	<i>Receipts from Cadastral and Technical Fees</i>	0	1,000 1,000	0	0
140368	<i>Miscellaneous Receipts</i>	0	1,000 1,000	0	0
	Jumla ya Kifungu	17,422,160	40,003,000	12,110,000	30.3
	Jumla ya Fungu 48	74,714,286,499.48	111,772,746,400	80,518,548,575.06	72.04

Jedwali Na. 2
MCANGANUO WA MATUMIZI YA KAWAIDA NA MIRADI YA MAENDELEO KATIKA MWAKA 2016/17

Aina ya Bajeti		Kiasi kilichoithin- ishwa 2016/17 baada ya uhamisho kufanyika (Reallo- cation)	Kiasi kili- chopokelewa hadi 15 Mei,2017	Kiasi kilichotu- mika hadi 15 Mei, 2017
1. Matumizi ya Kawaida	Mishahara	Mishahara ya Fungu bila Taasisi	12,220,512,600	11,607,793,700.75
		Mishahara ya Taasisi	1,892,901,750	1,013,554,250
	Jumla ya Mishahara		14,113,414,350	12,621,347,950.75
	Matumizi Mengineyo - OC	27,410,700,749	12,536,083,635.65	11,854,759,717.64
		1,442,594,000	678,255,370	678,255,370
	Jumla ya Matumizi Mengineyo	28,853,294,749	13,214,339,005.65	12,533,015,087.64
Jumla ya Matumizi ya Kawaida		45,196,085,749	27,327,753,356	25,154,363,038.39
2. Matumizi ya Maendeleo	Ndani	15,301,058,684.65	4,201,058,684.65	3,737,765,068.25
	Nje	10,000,000,000.00	3,425,160,629.63	3,425,160,629.63
Jumla Matumizi ya Maendeleo		25,301,058,684.65	7,626,219,314.28	82,626,014,813.05
Jumla ya Matumizi ya Kawaida na Matumizi ya Miradi		70,497,144,433.65	34,953,972,669.93	32,317,288,736.27

MIRADI YA UPIMAJI NA UMILIKISHAJI WA VIWANJA KATIKA MIJI MBALIMBALI NCHINI HADI 15 MEI 2017

Kanda	Mkoa	Halmashauri	Eneo Mradi Ulipo	Idadi ya Viwanja Katika Mradi	Bei ya Viwanja kwa Mita ya Mraba (Shilingi)			Taasisi Iliyopima na Kuuza
					Makazi	Makazi na Biashara	Matumizi Mengine	
					Shilingi	Shilingi	Shilingi	
Kanda ya Ziwa	Mwanza	Ilemela	Nyamikumilo	273	5000	5000	5000	Ardhiplan
			Fela	53	5000	5000	5000	Ardhiplan
			Kabusungu 'C' Phase I	320	4500	4500	4500	Sunset Es- tate Co.Ltd
			Kabusungu 'C' Phase II	162	2500	2500	2500	Sunset Es- tate Co.Ltd
			Masemele	274	4500	4500	4500	Sunset Es- tate Co.Ltd
			Kabusungu A	177	4500	4500	4500	Mashantaka Land Devel- opers Ltd

Kanda	Mkoa	Halmashauri	Eneo Mradi Ulipo	Idadi ya Viwanja Katika Mradi	Bei ya Viwanja kwa Mita ya Mraba (Shilingi)			Taasisi Iliyopima na Kuuza
					Makazi	Makazi na Biashara	Matumizi Mengine	
					Shilingi	Shilingi	Shilingi	
			Kabusungu B	36	4500	4500	4500	Mashantaka Land Developers Ltd
		Sengerema	Bujora	1231	2200	2500	1600 2600 3500	UTT Project And Infrastructure Development & Sengerema District Council
	Kagera	Bukoba (H/W)	Kemondo	13	2600	2800	2600	Halmashauri ya Wilaya

Kanda	Mkoa	Halmashauri	Eneo Mradi Uliipo	Idadi ya Viwanja Katika Mradi	Bei ya Viwanja kwa Mita ya Mraba (Shilingi)			Taasisi Iliyopima na Kuuza
					Makazi	Makazi na Biashara	Matumizi Mengine	
					Shilingi	Shilingi	Shilingi	
		Kyerwa	Rubwera - Kageyi	328	1500	2000	1800, 4000 na 6000	Halmashauri ya Wilaya
			Buhembe	748	3000	3300		BMC/UTT
			Nshamba	532	3000	3300		BMC/UTT
			Ihungo	141	3400	3600		BMC/UTT
			Nyanga	499	3000	3300		BMC/UTT
			Kagondo	456	3400	3600		BMC/UTT
			Kyasha	233	3000	3000		BMC/UTT
			Rwazi	124	3000	3300		BMC/UTT
			Rwome	128	3000	3300		BMC/UTT
			Mugeza	310	3000	3300		BMC/UTT
			Makongo	178	4000	4500		BMC/UTT
			Ijuganyondo	85	3000	3300		BMC/UTT

Kanda	Mkoa	Halmashauri	Eneo Mradi Uliipo	Idadi ya Viwanja Katika Mradi	Bei ya Viwanja kwa Mita ya Mraba (Shilingi)			Taasisi Iliyopima na Kuuza
					Makazi	Makazi na Biashara	Matumizi Mengine	
					Shilingi	Shilingi	Shilingi	
	Geita	Mbogwe	Bwelwa	853	800	800	1000	Interland Surveyors Co. Ltd
			Bugegele (Kagiri) Mjini Masumbwe	686	1800	2000	2000	Amboni Land Consultant Ltd
Jumla ya Kanda ya Ziwa				7840				

Kanda	Mkoa	Halmashauri	Eneo Mradi Uliipo	Idadi ya Viwanja Katika Mradi	Bei ya Viwanja kwa Mita ya Mraba (Shilingi)			Taasisi Iliyopima na Kuuza
					Makazi	Makazi na Biashara	Matumizi Mengine	
					Shilingi	Shilingi	Shilingi	
Kanda ya Kusini	Mtwara	Newala	Julia	136	3,000	-	2,000	Spatial Engineering Company
		Newala	Machinjioni	430	2,000	-	-	Mkurugenzi wa Hal-mashauri ya Mji wa Newala
	Lindi	Mji Wa Nanyamba	Kilimanjaro	194	1,700	2,500	7,000	Mkurugenzi wa Hal-mashauri ya Mji wa Nanyamba
		Lindi Manispaa	Ngongo	2,090	3,500	4,500	7,000	Mkurugenzi wa Hal-mashauri ya Manispaa ya Lindi

Kanda	Mkoa	Halmashauri	Eneo Mradi Uliipo	Idadi ya Viwanja Katika Mradi	Bei ya Viwanja kwa Mita ya Mraba (Shilingi)			Taasisi Iliyopima na Kuuza
					Makazi	Makazi na Biashara	Matumizi Mengine	
					Shilingi	Shilingi	Shilingi	
		Lindi Manispaa	Mitwero Kilimani	149	3,450	4,025	-	Surety Properties Company Limited
Jumla kwa Kanda ya Kusini				2,999				
Kanda ya Kaskazini	Tanga	Korogwe Mji	Bagamoyo	1,500	2,000	2,000	8,000	H/Mji
			Kilole	100	8,000	12,000	9,000	H/Mji
		Pangani	Mkoma	24	2,000	2,200		H/Wilaya
			Fungoni	52	2,000	2,200		H/Wilaya
		Lushoto	Kwesimu	410	4,000	6,500	3,000	H/Wilaya & Lushoto Coffee Growers Association

Kanda	Mkoa	Halmashauri	Eneo Mradi Uliipo	Idadi ya Viwanja Katika Mradi	Bei ya Viwanja kwa Mita ya Mraba (Shilingi)			Taasisi Iliyopima na Kuuza
					Makazi	Makazi na Biashara	Matumizi Mengine	
					Shilingi	Shilingi	Shilingi	
		Ngorongoro	Wasso	294	750	1,200	1,300	H/Wilaya
	Arusha	Meru	Madirra	233	10,000	10,000	25,000	H/Wilaya
		Arusha Jiji	Mateves (Safari City)	1,800	35,000	42,000	45,000	N.H.C.
	Kiliman-jaro	Mwanga	Mtalang'a	731	2,000	2,500	3,000	H/Wilaya
		Manyara	Babati Mji	Maisaka Katani	12,241	1,500	3,000	5,000
Jumla kwa Kanda ya Kaskazini				17,385				

Kanda	Mkoa	Halmashauri	Eneo Mradi Ulipo	Idadi ya Viwanja Katika Mradi	Bei ya Viwanja kwa Mita ya Mraba (Shilingi)			Taasisi Iliyopima na Kuuza
					Makazi	Makazi na Biashara	Matumizi Mengine	
					Shilingi	Shilingi	Shilingi	
Kanda ya Magharibi	Shinyan- ga	Kahama	Busoka/ Lugera	254	2500	2500	2500	Tupange Makazi Land Con- sult
					3500	4000	3500	Coonred Land Con- sult
			Busoka	570	3500	4000	3500	Mwenga Real Estate
					4000	4000	3000	UTT
			Ugweto	1014	2500	2500	2500	Mkurugenzi wa Hal- mashauri ya Manispaa ya Shinyan- ga
					4000	4000	2500	

Kanda	Mkoa	Halmashauri	Eneo Mradi Ulipo	Idadi ya Viwanja Katika Mradi	Bei ya Viwanja kwa Mita ya Mraba (Shilingi)			Taasisi Iliyopima na Kuuza
					Makazi	Makazi na Biashara	Matumizi Mengine	
					Shilingi	Shilingi	Shilingi	
			Mwalugoye	404	2500	2500	2500	Mkurugenzi wa Hal- mashauri ya Manispaa ya Shinyan- ga
			Mwasenga	552	2500	2500	2,000	Mkurugenzi wa Hal- mashauri ya Manispaa ya Shinyan- ga

Kanda	Mkoa	Halmashauri	Eneo Mradi Ulipo	Idadi ya Viwanja Katika Mradi	Bei ya Viwanja kwa Mita ya Mraba (Shilingi)			Taasisi Iliyopima na Kuuza
					Makazi	Makazi na Biashara	Matumizi Mengine	
					Shilingi	Shilingi	Shilingi	
Tabora	Masanga	Igunga		258	1,500	2000	1,500	Mkurugenzi wa Hal- mashauri ya Mji wa Igunga
					2,000	2500	2,000	Mkurugenzi wa Hal- mashauri ya Mji wa Igunga
	Uledi		7000	2,000	2500	2,000	Ardhiplan	
	Kariakoo		1600	1,500	2,000	1,500	Applied Ge- odes LTD	

Kanda	Mkoa	Halmashauri	Eneo Mradi Uliipo	Idadi ya Viwanja Katika Mradi	Bei ya Viwanja kwa Mita ya Mraba (Shilingi)			Taasisi Iliyopima na Kuuza
					Makazi	Makazi na Biashara	Matumizi Mengine	
					Shilingi	Shilingi	Shilingi	
			Bushabani	370	2,500	2,500	2,500	Ardhiplan
	Kigoma	Kigoma Manispaa	Mwasenga	149	3,450	4,025	-	Mkurugenzi wa Hal-mashauri ya Manispaa ya Kigoma
Jumla kwa Kanda ya Magharibi				13,804				
Kanda ya Mashariki	Moro-goro	Manispaa ya Morogoro	Mkundi	160	5,000	5,500	5,500	Manispaa ya Moro-goro
			Mkundi	297	5,000	5,500	5,500	LIPAZ

Kanda	Mkoa	Halmashauri	Eneo Mradi Ulipo	Idadi ya Viwanja Katika Mradi	Bei ya Viwanja kwa Mita ya Mraba (Shilingi)			Taasisi Iliyopima na Kuuza
					Makazi	Makazi na Biashara	Matumizi Mengine	
					Shilingi	Shilingi	Shilingi	
			Kiegea - Man- goroma	525	4,000	4,500	5,000	UTT
			Kingolwira	292	7,500	7,500	7,500	UTT
			Mkundi West	100	5,500	6,000	6,000	Florence Rweyemamu Francis
			Mkundi	73	5,500	5,500	5,500	Francis Zangiza
			Madanganya Mindu	390	7,500	7,500	7,500	UTT

Kanda	Mkoa	Halmashauri	Eneo Mradi Uliipo	Idadi ya Viwanja Katika Mradi	Bei ya Viwanja kwa Mita ya Mraba (Shilingi)			Taasisi Iliyopima na Kuuza
					Makazi	Makazi na Biashara	Matumizi Mengine	
					Shilingi	Shilingi	Shilingi	
			Zegereni Kitalu "J"	544	5,000	5,500	3,500	Kampuni Ya Geoffson's Investment Limited
			Visiga Kitalu "K"	320	6,000	6,500	3,500	Land General Limited
			Simbani Kitalu "G"	55	6,900	7,000	NIL	Josiah Stephano Gunda
			Kumba Kitalu "A"	49	6,900	7,000	NIL	Josiah Stephano Gunda
			Halmashauri Ya Miji Kibaha	14			8,000	Florence Rweyemamu Francis

Kanda	Mkoa	Halmashauri	Eneo Mradi Uliipo	Idadi ya Viwanja Katika Mradi	Bei ya Viwanja kwa Mita ya Mraba (Shilingi)			Taasisi Iliyopima na Kuuza
					Makazi	Makazi na Biashara	Matumizi Mengine	
					Shilingi	Shilingi	Shilingi	
			Magawa	116	3,000	3,500	4,000	Halmashauri ya Wilaya Mkuranga
			Magoza	540	5,000	5,500	5,000	Ena Land Consult Ltd
		Mkuranga	Mkwalia Kitumbo	250	5,000	6,000	8,000	Demarcation Real Estate
			Nganje	406	5,000	6,000	8,000	Demarcation Real Estate
			Tengelea	193	6,000	6,000	6,000	Makazi Solution
			Dondwe	530	5,000	6,500	8,000	Ardhiplan
			Miamleni	116	5,000	6,500	8,000	Ardhi Plan

Kanda	Mkoa	Halmashauri	Eneo Mradi Uliipo	Idadi ya Viwanja Katika Mradi	Bei ya Viwanja kwa Mita ya Mraba (Shilingi)			Taasisi Iliyopima na Kuuza
					Makazi	Makazi na Biashara	Matumizi Mengine	
					Shilingi	Shilingi	Shilingi	
			Mdimni	117	8,000	10,000	10,000	Arena Real Estate Developers Co. Ltd
			Palacha	126	15,000	18,000	18,000	Global Land Solution Co. Limited
			Mkokozi	127	5,500	6,000	8,000	Makazi Solution
			Mkwalia	132	8,000	8,000	8,000	Makazi Planners
			Kitonga	228	5,500	6,000	65,000	Jm International Co. Limited
				2,881				

Kanda	Mkoa	Halmashauri	Eneo Mradi Uliipo	Idadi ya Viwanja Katika Mradi	Bei ya Viwanja kwa Mita ya Mraba (Shilingi)				Taasisi Iliyopima na Kuuza
					Makazi	Makazi na Biashara	Matumizi Mengine	Shilingi	
					Shilingi	Shilingi	Shilingi	Shilingi	
			Mataya	215	8,800	10,000	10,000	10,000	Wellington Developers
			Mataya	144	6,800	7,000	7,000	10,000	Wellington Developers
		Bagamoyo	Kimalang'ombe	175	9,000	10,000	10,000	10,000	Bin Shaban Properties
			Mataya	85	7,000	7,000	7,000	7,000	Good Shepherd School
			Mataya	41	7,000	7,000	7,000	7,000	Maura Farm House
				660					
			Kiluvya	492	15,000	17,000	17,000	20,000	NSSF
		Kisarawe	Visegese	291	NIL	NIL	NIL	10,000	Wananchi
			Makurunge	173	6,500	7,000	7,000	5,000	Land Unit Ltd

Kanda	Mkoa	Halmashauri	Eneo Mradi Uliipo	Idadi ya Viwanja Katika Mradi	Bei ya Viwanja kwa Mita ya Mraba (Shilingi)			Taasisi Iliyopima na Kuuza
					Makazi	Makazi na Biashara	Matumizi Mengine	
					Shilingi	Shilingi	Shilingi	
		Makurunge		149	6,500	7,000	5,000	Ido Omari Isoki & Ignas Levira
		Visegese		135	5,000,	5,000	5,000	Abogast B. Mkwizu & Ignas Levira
Jumla kwa Kanda ya Mashariki				11,141				
Kanda ya Dar es Salaam	Dar es Salaam	Ilala	Msongola	2400	10,000	12,000	8,000	Tanzania Lemets Center
		Kigamboni	Lingato	83	10,000	10,000	10,000	Datum
			Lingato	285	10,000	10,000	10,000	Datum
			Lingato	66	10,000	10,000	10,000	Datum
		Lingato	149	10,000	10,000	10,000	Datum	

Kanda	Mkoa	Halmashauri	Eneo Mradi Uliipo	Idadi ya Viwanja Katika Mradi	Bei ya Viwanja kwa Mita ya Mraba (Shilingi)			Taasisi Iliyopima na Kuuza
					Makazi	Makazi na Biashara	Matumizi Mengine	
					Shilingi	Shilingi	Shilingi	
		Kigamboni	Lingato	511	10,000	10,000	25,000	Geo Plan Designe
			Lingato	267	10,000	10,000	10,000	Tafsus
			Lingato	123	10,000	10,000	10,000	Michael Clement Juma
			Lingato	51	18,000	18,000	18,000	Malima
			Lingato	152	20,000	20,000	20,000	Imara Soft-ware
			Tundwi	132	20,000	20,000	20,000	Imara Software
			Lingato	220	8,500	8,500	8,500	Ardhiplan
			Potea	151	8,500	8,500	8,500	Ardhiplan
			Buyuni	223	8,500	8,500	8,500	Ardhiplan

